MID WEEK JACKPOT!
TZS. 544,830,140
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Serikali** yatoa ufafanuzi vyura wa Kihansi

UKURASA 4


Wadau wa elimu wakusanyika kutafakari kuongeza uwezo HESLB
Nipashe
TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Taasisi ya Ustawi wa Jamii yawafunda sumu ya pombe, 'unga' kwao na abiria
ELIMU
NA NEEMA HUSSEIN, MPANDA
Kundi wanaofeli kidato cha pili Katavi wanakimbia kurudia wakikwepa aibu
• Wakuu shule wabuni staili yao kuwarejesha

UKURASA 11

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumanne Aprili 11, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581277

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## CAG abaini mapato mifuko NSSF, PSSSF yashuka

UK. 2

# Samia apongezwa

• **Ni** kuhusu Ripoti ya CAG, wadau wasema hatua aliyochukua ni sahihi, lakini... *Endelea Ukurasa 2*





Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye pia ni Mbunge wa Rufiji, Mohamed Mchengerwa, akigawa chakula wakati alipotoa sadaka ya futari kwa zaidi ya waumini 8000 wa dini ya Kiislam wilayani Rufiji, mkoani Pwani juzi, ambapo pia aliungana nao kufanya dua maalum ya kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan na Taifa. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

## Ajali yaua 13 wakitoka mnadani

UK. 2




Kampuni ya the Guardian Limited, Wachapishaji wa Magazeti ya the Guardian na Nipashe, inawakaribisha wadau wote wa maendeleo kutoa salaam za pongezi wakati tunaadhimisha miaka 59 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Toleo hili litachapishwa tarehe 26 Aprili, 2023 kwenye Magazeti ya Guardian na Nipashe.

The Guardian
Nipashe

Kwa mawasiliano zaidi,
Tupigie +255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

MICHEZO YANGA YATAMBA KIKOSI KIPANA UK.24 MAONI UK.6



Mwenyekiti wa Bodi ya E. Merck KG na Bodi ya Wadhamini ya Merck Foundation, Prof. Frank Stangenerg-Haverkamp na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Merck Foundation, Seneta Dk. Rasha Kelej, wakiwa pamoja na Mwandishi wa Habari, Christina Mwakangale (katikati) aliyeibuka mshindi wa kwanza kwa nchi za Afrika Mashariki wa tuzo ya 'Diabetes and Hypertension Media Recognition Awards 2022' kipengele cha magazeti (Tanzania Daima), katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wapongeza hatua ya Samia

**Na Elizabeth Zaya**

SIKU moja baada ya Rais kutoa maelekezo kwa Katibu Mkuu Kiongozi kuhakikisha Makatibu Wakuu na Watendaji Wakuu wote wa Taasisi za serikali wanaipitia kwa kina taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ili kujibu na kuzifanyia kazi kwa haraka hoja zote zinazogusa maeneo yao, wadau wamepongeza hatua hiyo na kutaka kazi zaidi ifanyike

Juzi Rais Samia Suluhu Hassan Rais Samia alivunja Bodi ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) na kutengua uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA), Mhandisi John Nzulule.

Pia, alimuelekeza Katibu Mkuu Kiongozi kuhakikisha kuwa makatibu wakuu na watendaji wakuu wote wa taasisi za serikali wanaipitia kwa kina taarifa ya CAG, kujibu na kuzifanyia kazi kwa haraka hoja zote zinazogusa maeneo yao.

Akizungumza na gazeti hili, CAG mstaafu Ludovick Utouh, alisema hatua ya Rais ni ujumbe sahihi kwa wakati sahihi kwa wenyeviti wa bodi na wakurugenzi wa taasisi za serikali kwamba zinaendeshwa kwa mali za umma na zinatakiwa zitumike kwa maslahi ya umma na sio watu binafsi.

Alisema kwa maoni yake hatua ya Rais Samia ni mwanzo wa hatua zaidi kwa kuwa hachukui hatua kwa sababu CAG kasema bali ana taasisi zinazomshauri. "Naamini hii ni hatua ya mwanzo, nyingi zaidi zinakuja."

"Taasisi zipo kwa niaba ya umma na rais anazimiliki kwa niaba ya Watanzania, anavyochukua hatua anawakilisha wananchi," alisema Utouh CAG mstaafu aliyefanyakazi hiyo toka mwaka 2006 hadi 2014.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema kuna haja ya kuwa na mifumo imara, Katiba mpya na maadili kwa wa watumishi wa umma na kuhakikisha wapinzani wanapata nafasi katika nafasi za uamuzi kama Bunge ili kusaidia kusimamia na kuhoji matumizi ya rasilimali za nchi.

"Ni hatua nzuri anayofanya rais, lakini vita vya rushwa vinapaswa kupiganwa na mifumo, na inapaswa kupiganwa na kila mtu kunzia ngazi ya halmashauri, taasisi mbalimbali za serikali mpaka serikali kuu."

"Sasa ukiangalia mifumo ya ufuatiliaji na uwajibikaji ina changamoto, nchi haiwezi kupigana na rushwa kwa kutegemea mtu mmoja, bunge linapaswa kuwa na kiwango kikubwa cha ufuatialiaji wa uwajibikaji, hakuna njia nyingine ya kuwawajibisha zaidi ya bunge.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shule Kuu ya Elimu (DUCE), Dk. George Kahangwa, alisema hatua iliyochukuliwa na Rais Samia ni nzuri huku akiomba hatua zaidi ili kumaliza tatizo."Hatua aliyochukua Rais Samia ni nzuri sana, lakini sio hiyo peke yake inayotakiwa kuchukuliwa. Kwanza taarifa ya Ikulu inataja habari ya serikali kuu na watendaji wakuu wa idara zake. Hapo haijagusa maeneo mengine yanayotajwa katika ripoti ya CAG. Kuna serikali za mitaa, miradi, vyama vya siasa na kwingine, huko nako kunahitaji hatua inayotoka kwenye mamlaka kubwa," alisema Dk. Kahangwa.

"Aidha, taarifa ya Ikulu inasema kushughulikia haraka. Kama ni muda uliotolewa, basi uwe wazi, Watanzania wajue kuwa labda ni mpaka ifikapo mwisho wa mwezi Mei mwaka huu au lini, uwekwe muda maalum wa kushughulikiwa suala hilo aliloelekeza Rais Samia."

Pia, alisema ni vyema hata Katibu Mkuu Kiongozi apewe tarehe ya kuleta mrejesho wa maagizo hayo hadharani.

"Lakini pia shida iliyopo kwenye maagizo hayo ni kwamba. Je kama kuna Katibu fulani naye ni mhusika wa dudu mojawapo kati ya yaliyotajwa kwenye ripoti. Kusoma tu ripoti hakutatosha, kama hatasimama kwanza ili achunguzwe," alitahadharisha Dk. Kahangwa.

Alisema pia ni vyema Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) naye akachukua hatua pasipo kusubiri kuagizwa.

"Kwa kuwa serikali za mitaa zinasimamiwa na Waziri wa TAMISEMI, bora naye pengine bila kusubiri kuagizwa, achukue hatua kwa mujibu wa mamlaka aliyopewa," alisema Dk. Kahangwa.

Alipendekeza ni vyema msomaji mkuu wa ripoti hiyo ya CAG angekuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ili naye aseme anachukua hatua gani na lini kuhusu ubadhirifu uliobainika katika ripoti hiyo.

Mwingine ambaye alisema anatakiwa atoke hadharani na kusema hatua anazozichukua ndani ya mamlaka yake kuhusu ripoti ya CAG, ni Msajili wa Vyama vya Siasa na kwamba rais aendelee kusikiliza maoni ya wadau ya nini kifanyike.

Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Mahusiano na Umma wa Chama Cha Wananchi (CUF), Mohamed Ngulangwa, alipendekeza kuwa mwarobaini wa ubadhirifu huo ni kurudi kwenye utaratibu wa kuheshimu sheria ya ununuzi na kanuni zake.

"Haya yote yanatokana na uamuzi mbaya wa serikali wa kutumia force account kwenye miradi kadhaa kwa kuwa yanakiuka misingi ya ushindani katika zabuni na kuchochea ufisadi na kutowajibika," alisema Ngulangwa.

Pia, alitaka uchunguzi wa kina ufanyike ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa wahusika na kupendekeza kuwapo kwa kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kuisaidia kuimarishwa kwa kila taasisi ya umma.

## 13 walivyofariki dunia ajalini

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WAFANYABIASHARA 13 wamefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kutoka mnadani eneo la Ndongosi kuelekea Kijiji cha Namatuhi, kupinduka na kuangukia Mto Njoka, Songea Vijijini, mkoani Ruvuma.

Akizungumza na waandishi wa habari Hospitali ya Serikali ya Mkoa Songea (HoMSO) ambako wakazi wa Songea mjini walifika kutambua maiti za ndugu zao, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Marco Chilya, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa tatu usiku.

Alisema wafanyabiashara watatu kati yao wamelazwa katika Kituo cha Afya cha Mpitimbi, wilayani Songea wakiendelea na matibabu.

Kwa mujibu wa Kamanda, gari hilo lenye namba za usajili T800 BXB aina ya Mitsubishi Fusso lililokuwa likiendeshwa na Thobias Njovu, lilipofika kwenye daraja la mto huo lilipanda mlima na kuacha njia na kutumbukia mtoni.

Aliwataja waliofariki kuwa ni Happy Msemwa, Jafari Ngalimus, Hidaya Salum, Biesha Yahaya, Mustafa Ally na wengine waliofahamika kwa jina moja moja ni Mwaisha, Hamad, Juma Said, Boniface, Christopher Msuya, Deograsia Mapunda, Simba na mama Faraja.

Wanaoendelea na matibabu ni Hamis Mbawala na Christofa Banda na kwamba miili ya waliofariki dunia kwenye ajali hiyo imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Mkoa wa Songea.

Kamanda Chilya, aliwataka wananchi kuacha kutumia magari ya mizigo wanapokwenda kwenye shughuli zao na mnada na kwamba hatua kali zitachukuliwa kwa wanaohusika.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Serikali ya Mkoa wa Songea, Dk. Magafu Majura, alithibitisha hospitali hiyo kupokea miili 13, wakiwamo wanawake saba na wanaume sita.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, akiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama walifika eneo la kuhifadhia maiti na kutoa pole kwa wafiwa waliofika kutambua miili ya wapendwa wao.

Akizungumza na wananchi hao, alisema serikali ilishatoa katazo muda mrefu la wafanyabiashara wanaokwenda kwenye minada kupanda gari moja na mizigo.

Mmoja wa ndugu wa marehemu wa ajali hiyo, Nestory Nyanguru, mkazi wa Subira Manispaa ya Songea, alisema walitambua mwili wa mdogo wake ambaye alikwenda mnadani.

HABARI KITAIFA

# CAG abaini mapato mifuko NSSF, PSSSF yashuka

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), imebaini kushuka kwa viwango vya mapato kwa miradi iliyo chini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Ripoti ya mwaka ya ukaguzi wa ufanisi ya 2021/22, ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) ilibaini kulikuwa na kushuka kwa viwango vya mapato hadi asilimia 81 kutoka 96 katika mwaka wa fedha 2017/18, na hadi asilimia 15 kwa mwaka wa fedha 2021/22 kwa jengo la Water Front.

Huku, Julius Nyerere Pension Tower, mapato yakishuka hadi asilimia 75 kutoka 95 mwaka wa fedha 2017/18; na hadi asilimia 20 kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Aidha, CAG alibaini kuwa PSSSF kiwango cha mapato kilibainika kushuka kutoka asilimia 28 katika mwaka wa fedha 2017/18 hadi 21 katika mwaka wa fedha 2021/22.

Kuhusu kuwapo kwa majengo ya uwekezaji yenye hali isiyoridhisha, ripoti hiyo ilieleza ukaguzi ulibaini kuwapo kwa majengo chakavu na yaliyokuwa katika hali mbaya yanayomilikiwa na PSSSF na NSSF.

"NSSF, dosari zilizobainika ni pamoja na nyufa kwenye sakafu na kuta, dari mbovu, fangasi ukutani na rangi za ukutani kung'olewa, paa kuvuja na kuvunjwa kwa madirisha, madoa kwenye mbao za dari, vyoo na milango mibovu, kuharibika kwa milango.

"Kwa upande wa PSSSF, kasoro zilizobainika ni nyufa, kuchubuka kwa rangi kwenye kuta, kuvuja kwa paa, kupasuka na kuchakaa kwa sakafu, kutu kwenye mabati, mfumo mbovu wa majitaka, ubovu wa lifti na uchakavu wa nyaya za umeme.

"Ukaguzi pia ulibaini kulikuwa na majengo yenye hali chakavu, ambayo yalitelekezwa kama vile Mradi wa Nyumba za Makazi Dege na Mradi wa Nyumba Kijichi."

Kwa mujibu wa CAG, hali mbaya ya majengo ilichangiwa na ufinyu wa bajeti na kutoendeshwa kwa shughuli za matengenezo, hali iliyosababisha kutofanyika kwa matengenezo ya kutosha kwa majengo hayo.

CAG amebaini majengo yaliyochakaa yalisababisha idadi ndogo ya watu kukaa au kutokaliwa kwa majengo hayo, hivyo kusababisha kushuka kwa kiwango cha mapato.

**MALI ZISIZOHAMISHIKA**

Aidha, ripoti hiyo ilibaini kuwa baadhi ya uwekezaji wa mali za NSSF haukuwa na faida na kwamba ulifanya uwekezaji wa mali usio na faida wa jumla ya Sh. 323,566,201.

Sambamba na hilo, kulikuwa na miradi 10 ya uwekezaji wa majengo, ambayo haikukamilika kwa matumizi na baadhi kutelekezwa na jumla ya Sh. 3,305,397,599 zilibainika kuwa uwekezaji usio na faida PSSSF.

Miradi hiyo ni Kiwanja cha Biashara na Makazi cha Ununio jijini Dar es Salaam na Nyumba za Makazi Njedengwa, jijini Dodoma.

"Sababu za kutofanikiwa kwa miradi hiyo ni mipango duni ya miradi na kushindwa kukamilika ndani ya muda uliopangwa hali iliyosababisha mabadiliko ya mwelekeo wa uwekezaji kutoleta mapato kwa mifuko.

"Kadhalika, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na kiwango kidogo cha mapato kurudisha faida kwenye uwekezaji wa mali zisizohamishika. Ufanisi wa mapato kurudisha faida kwenye uwekezaji wa mali isiyohamishika kwa PSSSF ulifikia asilimia 70.43 katika mwaka wa fedha 2019/2020 kisha hadi asilimia 21.90 katika mwaka wa fedha 2021/2022. Kushuka kwa mapato kulifikia asilimia 48.53 kwa miaka mitatu ya fedha iliyopita," ilifafanua.

CAG alibainisha kuwa mapato hayo yalishuka kwa kasi kutoka asilimia 70.43 mwaka 2019/20 hadi asilimia 17.76 mwaka wa fedha 2020/21 sawa na asilimia 52.67.

Vilevile, kwa NSSF mapato yatokanayo na uwekezaji wa majengo yalikuwa ya wastani wa asilimia 1.83 kwa miaka minne iliyopita ambayo ni chini ya asilimia tisa ya uwekezaji kwenye dhamana za serikali, ambayo ina asilimia 10.83 kama faida ya wastani ya uwekezaji.

Kwa upande mwingine, Ripoti za Usimamizi wa Miliki za PSSSF za mwaka wa fedha 2021/22, zilionesha kuwa, gharama za uendeshaji wa majengo ya uwekezaji zilikuwa juu zaidi ikilinganishwa na tozo ya huduma iliyokusanywa. Gharama za huduma zilizokusanywa hazikutosha ikilinganishwa na gharama za uendeshaji wa majengo.

CAG alibaini jengo la Golden Jubilee, lilitumia Sh. milioni 226.97 kama gharama za uendeshaji, huku makusanyo ya ada ya huduma yakiwa Sh. milioni 196.73.

Jengo la Twin Tower lilitumia Sh. milioni 245.65 kama gharama za uendeshaji, huku makusanyo yatokanayo na ada ya huduma yakiwa Sh. milioni 96.81.

Kwa mujibu wa CAG, ongezeko la gharama za uendeshaji wa majengo zilisababishwa na ukusanyaji usioridhisha wa ada za huduma na kupungua kwa idadi ya wapangaji katika majengo.


**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**SAID ROBERT KONYA** anatangaza Kupotea kwa Kadi ya PIKIPIKI Yenye namba za Usajili **DAU MC 765** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo Cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOD/DOD/RB/163585/2022.**



**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NA. 212 MWAKA 2022**

**THE ENERGY AND WATER UTILITIES REGULATION AUTHORITY** ..................................................................**MDAI**

**DHIDI YA**

**EAST AFRICAN FOSSILS COMPANY LIMITED** .................................**MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

**Kwa:**

**EAST AFRICAN FOSSILS COMPANY LIMITED**

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la madai dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati za madai zinazopatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 09/05/2023 saa mbili na nusu (08:30) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Jaji S.M.Maghimbi, kwa ajili ya kujibu madai hayo dhidi yako.

**ANGALIA**

Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa ulipokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wenu. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kutumia katika utetezi wako siku hiyo.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe ........30......... mwezi ......March....... 2023.

THE HIGH COURT OF TANZANIA

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**

217361502



**The United Republic of Tanzania**
**President's Office**
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

**VACANCY ADVERTISEMENT**

Tanzania Social Action Fund (TASAF) is currently implementing Productive Social Safety Net Program which aims at protecting the Vulnerable Poor Households from severest consequences of poverty by implementing interventions that will lead to increased household incomes and opportunities while increasing consumption.

The TASAF Executive Director is inviting applications from suitably qualified Tanzanian nationals to fill the below vacant posts:-

1. Director of Knowledge Management and Advocacy 1 post
2. Communication Specialist 1 post

Job Descriptions and required qualifications for these posts are available in TASAF website www.tasaf.go.tz

**How to apply**;

1) a) Applications, enclosing scanned certified copies of certificates and Curriculum Vitae be sent to the following address:-
**Executive Director**
**Tanzania Social Action Fund (TASAF) Kambarage Tower Building**
**Jakaya Mrisho Kikwete Road**
**P.O. Box 2719**
**DODOMA.**
b) Applications (In PDF Format), enclosing scanned certified copies of certificates and Curriculum Vitae be sent through the following email address: **hr@tasaf.go.tz**
2) Applications made in a way other than the above will not be considered,
3) Deadline for receiving applications i**s 10th May, 2023.**

**Ladislaus J. Mwamanga**
**EXECUTIVE DIRECTOR**

217361201

# CHADEMA: Waliotajwa ripoti CAG wawajibishwe

**Na Jenifer Gilla**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetaka uwajibikaji kwa wote waliotajwa kwenye ubadhirifu na uhujumu wa fedha za umma kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Aidha, kimependekeza kuundwa kwa tume ya kijaji kuchunguza suala la kupotea pesa za malipo zilizotokana na watu waliokiri makosa (Plea Bargaining).

Akitoa uchambuzi wa Ripoti hiyo kwa waandishi wa habari jana, jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema wamegundua upungufu katika kuwawajibisha wabadhirifu waliotajwa katika ripoti, ikiwamo kuwaadhibu watendaji wa taasisi na kuwaacha viongozi wa juu wa wizara jambo linaloongeza mwanya wa kuendelea kutendeka kwa makosa hayo.

"Kwa namna ya pekee tunalitaja jina la aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka (DPP), ambaye kwenye Ripoti ya CAG, ametajwa kwa cheo Biswalo Mganga, kwamba huyu anapaswa kuchunguzwa na kuchukuliwa hatua na kwa kuwa kwa sasa ni jaji, Rais atumie mamlaka yake kuunda chombo kitakachowezesha kufanyika kwa kuchunguza na hatua kuchukuliwa," alisema.

Alisema chama kinatoa wito kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuwajibika kutokana na udhaifu na ubadhirifu na hasara kwa serikali uliofanyika katika kipindi cha miaka miwili ya fedha akiwa kama Mtendaji Mkuu na Msimamizi wa shughuli za serikali huku hotuba yake bungeni Aprili 5, haikuonyesha kusimamia mapendekezo yaliyotolewa na CAG ya mwaka 2020/2021.

Pia, alisema katika ripoti zote mbili za CAG ya mwaka 2020/2021 na 2021/2023 wamegundua kuwa serikali ilipaswa kuwachukulia hatua aliyekuwa Waziri wa Fedha, na Katibu Mkuu wake wa wakati huo, kwa kuwa baadhi ya mambo yaliyoonyeshwa kwenye ripoti hiyo yalitendeka chini ya uongozi wao. Alisema chama kinatoa wito kwa Bunge linaloanza leo, kutenga muda wa kujadili ripoti ya CAG kwa kuanza na ya mwaka 2020/2021 ambayo bado utekelezwaji wa mapendekezo yake haujakamilika pamoja na kutaka serikali ipeleke muswada wa marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi, ili kuondoa vikwazo vinavyosababisha ripoti kujadiliwa kwa haraka na bunge kama ilivyokuwa mwanzo.

Chama hicho kimesema kutochukuliwa hatua madhubuti kwa waliohusika kila mwaka kumeitia hasara nchi na kuona ni jambo la kawada ndiyo maana CAG anabaini kasoro.

Katibu Mkuu huyo alisema uamuzi wa rais kuvunja Bodi ya TRC, peke yake kwa tuhuma za kuitia serikali hasara ya Sh. bilioni 503 hautoshi kwa kuwa mchakato wa kumpata mzabuni na kulipa malipo uliiuhusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa wakati huo na Wizara ya Fedha kwa barua ya Katibu Mkuu wa Hazina wa wakati huo.

Alimtaka rais kutoa muda wa ukomo kwa Makatibu wakuu waliotajwa kwenye ripoti za CAG, wajibu hoja zao kwa haraka na kama kuna kasoro yoyote hatua za kisheria zichukuliwe ili kuchelewesha mchakato wa kuwawajibisha wote waliopo kwenye mnyororo huo na kuepuka kulinda ufisadi.

Alisema wanatarajia kufanya mikutano ya hadhara ikiwa ni mwendelezo wa kutoa taarifa kwa jamii kuhusu ubadhirifu unaofanywa kwenye pesa wanazolipa kupitia kodi na tozo na kuwa matarajio ya Watanzania ni kuona pesa zao zinarudishwa, huku wahusika wote waliopo kwenye mamlaka za kiserikali kuondolewa na kupelekwa mbele ya vyombo vya sheria.




Kiongozi wa Chama cha ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana wakati wa uchambuzi wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), iliyolenga maeneo makuu 10. Kulia ni Waziri Kivuli wa Chama hicho, Sekta ya Uwekezaji, Mashirika ya Umma na Hifadhi ya Jamii, Mwanaisha Mndeme. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# ...ACT yataka wahusika waundiwe kamati

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema wahusika wote waliobainishwa kuhusika na ubadhirifu wa fedha za umma, waundiwe kamati teule ya Bunge na kuitwa kujieleza ili wachukuliwe hatua za kisheria kutokana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2021/2022 kubainisha kasoro za watendaji hao.

Aidha, kimesema kabla ya viongozi wahusika kuchukuliwa hatua, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, awajibike, kutokana na makosa ya ununuzi wa mabehewa ya Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) na ununuzi wa ndege za Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL).

Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe aliyasema hayo jana, jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uchambuzi wa ripoti hiyo ambayo chama hicho, kimezingatia maeneo 10 kutokana na umuhimu wake.

Alisema ripoti kadhaa za CAG miaka ya nyuma, zilibaini kuwapo kwa kasoro kwenye mashirika, ikiwamo katika Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2017 na Kanuni za mwaka 2013, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa ingawa kulitolewa mapendekezo.

Kadhalika, alisema Bunge lifanyie kazi hoja za ununuzi wa mabehewa ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa Spika wa Bunge kuunda kamati teule, ambayo itachunguza kwa kuwahoji wahusika sababu ya ya bei ya ununuzi kuongezeka.

Alisema pamoja na hoja za ukaguzi katika ripoti kuwa nyingi zikiwamo mpya na za nyuma, hazijafanyiwa kazi, akitaka serikali ya Rais Samia ianze kufanyika kazi na kuchukua hatua bila woga.

Kwa mapendekezo ya chama, Zitto alisema uchambuzi wa ACT-Wazalendo ilijikita katika hoja za msingi, ikiwamo hatari ya kufilisika kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) baada ya CAG kubaini kasoro kwa mara nyingine kutokana na mwaka huu wa ukaguzi kubaini Sh. bilioni 205 ni hasara. Kadhalika, kwenye upotevu wa mabilioni ya mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Zitto alisema CAG alibaini kupotea kwa Sh. bilioni 97.59 za mikopo hiyo, na kwamba ACT-Wazalendo inapendekeza kuwa mikopo hiyo itolewe kupitia Skimu ya Hifadhi ya Jamii.

Alisema wakati CAG akibaini TANROADS haikujenga barabara hata moja kwa mwaka 2021/2022 na kushindwa kutekeleza bajeti yake yote ya mwaka 2021/2022 licha ya kutengewa fedha na Bunge ya Sh. tril 2.9, Waziri wa Miundombinu Prof. Mbarawa ajiuzulu.

Kuhusu ATCL kukodisha ndege kutoka TGFA na CAG kubaini upungufu, hasara na hoja kadhaa za ukaguzi zinazohusu Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL). kwa mwaka 2021/22, huku Shirika hilo likipata hasara ya Sh. bilioni 35, chama hicho kimeshauri ndege zote zimilikiwe na ATCL.

Kuhusu Mradi wa Mabasi ya yaendayo haraka awamu ya pili, chama hicho kinaitaka DART kuingia mkataba mara moja na TPDC kubadilisha mabasi ya mwendokasi kutoka kutumia dizeli na kutumia gesi asilia (CNG).

Kadhalika, kwenye mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere, alisema chama kinapendekeza mawaziri wa Nishati, Madini na TAMISEMI wasimamie makubaliano ya mkataba unaoanza Julai, mwaka huu, ili wananchi wafaidike na hio CSR.

## Serikali yatoa ufafanuzi vyura wa Kihansi

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema mpango wa kuwarudisha vyura wa Kihansi waliopo nchini Marekani, ulianza kufanyika Desemba mwaka 2012 na tayari 2,500 wamerejeshwa nchini.

Pia limesema hadi kufikia mwaka 2019 zaidi ya vyura 12,000 walikuwa wamerejeshwa na matarajio Juni mwaka huu, wote watakuwa nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Shirika hilo, kwa sasa nchi imejijengea uwezo wa kuwahifadhi vyura hao katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Kihansi.

Uamuzi wa kupeleka vyura nchini Marekani ulifanywa na Wizara ya Nishati na Madini mwaka 2000, Waziri akiwa Abdallah Kigoda, mkataba uliisha mwaka 2020 na uliongezwa kwa miaka mwili wakati Waziri akiwa ni Dk. Medard Kalemani, ambao uliisha 2022.

"Mnamo mwaka 1996, iligundulika ni vyura wa kipekee ambao hawapatikani sehemu nyingine duniani isipokuwa katika bonde la Kihansi nchini Tanzania. Vyura hawa huzaa badala ya kutaga mayai kwa kuwa mayai hukaa ndani ya mwili wa chura hadi siku ya kuzaa," ilisema taarifa hiyo.

Ilieleza kwamba, vyura hao wanaishi kwenye mazingira ya maji yanayotiririka na kutoa mvuke au ukungu mwingi sana kutokana na nguvu ya maji na walikuwa wapo katika hatari ya kutoweka, hivyo nchi kwa makubaliano na maamuzi mawili yakiwa ni kuendelea na ujenzi wa mradi wa umeme na kuwalinda vyura wasipotee na kuendelea na ujenzi wa mradi wa umeme.

Aidha, taarifa hiyo iliongeza kwamba, hatua mbili zilichukuliwa ambazo ni kujenga miundombinu ya kuzalisha mvuke au ukungu, ili vyura hawa wasife, lakini kwa kuwa miundombinu hiyo haikuwa ya asili, iliamua kuwapeleka vyura 500 kwenye maabara nchini Marekani na UDSM. Aidha, taarifa ilisema kwamba mkataba wa vyura hao kuendelea kubakia nchini Marekani uliisha Juni 2020, lakini walishindikana kurudishwa nchini kwa sababu ya UVIKO-19 na hivyo mkataba uliongezwa muda hadi Juni, mwaka jana.

"Kama nchi tumepata faida kubwa za uwapo wa mradi huu kwani umekuwa ukisaidia katika upatikanaji wa umeme wa uhakika na wenye ubora pamoja na kuliingizia Shirika Sh. trilioni 3.4 ukilinganisha na matumizi yaliyofanyika."

Taarifa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mwaka 2021/2022 ilisema, mpango wa kuwarudisha vyura hao nchini ulishaanza kufanyika kuanzia Desemba 2012 na 2,500 walirudishwa nchini na hadi kufikia 2019, zaidi ya 12,000 walikuwa wamesharejeshwa nchini.

## TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

# MWITO WA KUTOA MAONI

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Afroil Investment Limited, S.L.P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 260 & 261, Kitalu "TC", Eneo la Ihumwa, Dodoma. | Hilmy Ahmed (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 2. | Njombe Filling Station Company Limited- Mafinga, S.L.P 411,Njombe | Kiwanja Na. 823, Kitalu "D", Eneo la Mafinga, Mufindi, Iringa. | James Malika Mwinuka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 3. | Asas Energies Limited – Kibwabwa, S.L.P 553,Iringa | Kiwanja Na. 51 Kibwabwa Industrial Area, Iringa. | Ahmed Faraj Abri (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 4. | Bageni Company Limited, S.L.P 586, Kahama. | Kijiji cha Kakola, Kahama, Shinyanga. | Manyengo Bageni Nyamrere (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya Mafuta |
| 5. | Jambo Food Products Limited, S.L.P. 71, Shinyanga. | Kiwanja Na. 12 & 13, Kitalu "LL", Eneo la Ibadakuli, Shinyanga. | Salum Khamis Salum (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 6. | Pirmohamed Enterprises, S.L.P 2567, Mwanza. | Mtaa wa Bulugalila, Shinyanga | Ayoub Aziz Pirmohamed (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa gesi ya kupikia (LPG) |
| 7. | Stamigold Company Limited, S.L.P 103, Biharamulo. | Kijiji cha Mavota, Biharamulo, Kagera. | Gilay Shamika (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 8. | Karagwe Oils Company Limited, S.L.P 484,Karagwe. | Kiwanja Na. 94, Kitalu "D" Kayanga, Karagwe, Kagera. | Seleman Zahor Mansoory (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 9. | Remigius Patrick Nshange, S.L.P 881, Bukoba. | Kijiji cha Mushozi, Kaagya, Bukoba, Kagera | Remigius Patrick Nshange (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 10. | Admire Oil Limited, S.L.P 7494, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 2, Kitalu "A", Iganjo, Mbeya. | Said Mire Artan (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 11. | Mtweve Oil – Yohana Edward Mtweve S.L.P 40 Chunya. | Kijiji cha Ifumbo, Chunya, Mbeya. | Yohana Edward Mtweve (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 12. | Manyanyas Oil Limited, S.L.P 132, Tunduma-Momba | Kiwanja Na. 18, Kitalu "H", Tunduma, Momba, Songwe. | Bahati Msajie Mnozya (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 13. | Puma Energy Tanzania Limited - Puma Sumbawanga Service Station, S.L.P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 150, Kitalu "H", Jangwani, Sumbawanga, Rukwa. | Fatma Mohamed Abdallah (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 14. | Salalah Petroleum Limited, S.L.P 15778, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "21", Eneo la Kariakoo, Ilala, Dar es Salaam. | Awadh Gharib Omar (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya mafuta |
| 15. | Patterson Group Limited, S.L.P 32292, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2, Eneo la Bunju, Kinondoni, Dar es Salaam. | Atu Patrick Mwakitwange. (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya mafuta |
| 16. | M/S Ospher International Limited, S.L.P 938, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.45, Kitalu "H", Eneo la Vingunguti, Ilala, Dar es Salaam. | Mehul J. Upadhyay. (Raia wa India) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi |
| 17. | Kobil Africana, S.L.P 16351, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2350, Kitalu "H", Eneo la Mbezi, Kinondoni, Dar es Salaam. | Yuda Peniel Mosha (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 18. | Peter Saroni, S.L.P 9103, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.135, Eneo la Mtoni Mtongani, Temeke, Dar es Salaam. | Jean Francois Schoepp (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 19. | Puma Energy Tanzania Limited, S.L.P 9043,Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 255/1 &256/1, Kitalu "B", Eneo la Vingunguti, Ilala, Dar es Salaam. | Fatma Mohamed Abdalah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 20. | GAPCO Banana Service Station- Ukonga S.L.P 1503,Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1361-4/1, Kitalu "C", Eneo Ukonga, Ilala, Dar es Salaam. | Ellon Kanyingi Kamau. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 21. | Big Bon New Msimbazi Co. Ltd – Kariakoo, S.L.P 21531, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 10-17, Kitalu "13", Eneo la Kariakoo, Ilala, Dar es Salaam. | Mohamed Salim Bahashwan (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 22. | Giraffe Oil Company Limited, S.L.P 79342, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1205, Kitalu "F", Eneo la Magogoni, Kigamboni, Dar es Salaam. | William Jackson Nyakua (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 23. | Darpco Energy Limited - Kongowe Petrol Station S.L.P 3892, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 7, Kitalu "D", Eneo la Kongowe, Temeke, Dar es Salaam. | Thabit George Mkasi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 24. | Lodhia Industries Limited, S.L.P 12167, Arusha. | Kiwanja Na. 6/1, Kitalu "B", Eneo la Kisemvule, Mkuranga, Pwani. | Arlen Vithaldas Lodhia . (Mtanzania) | Leseni ya Mafuta ya Matumizi Binafsi. |
| 25. | Animal Care Company Limited, S.L.P 55010, Pwani. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "E", Eneo la Vikuruti, Wilaya ya Kibaha, Mkoa wa Pwani. | Hafidh Hamdoun Mansour. (Mtanzania) | Leseni ya Mafuta ya Matumizi Binafsi. |
| 26. | Msata Five Star Station S.L.P 67, Pwani. | Kiwanja Na. 2, Eneo la Msata, Bagamoyo, Pwani. | Mohamed Iqbal Gulamhussein. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 27. | Athumani Juma Digaga T/A Mloka Filling Station S.L.P 28, Pwani. | Kiwanja Na. 178, Eneno la Mwaseni, Mloka, Rufiji, Pwani | Athumani Juma Digaga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 28. | Afroil Investment Limited, S.L.P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 343, Kitalu "B", Eneo la Kichangani,Morogoro. | Hilmi Ahmed Mbaraka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 29. | Puma EnergyTanzania Limited. S.L.P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 184,185 and 186, Kitalu "H", Eneo la Rahaleo, Mtwara. | Fatma Mohamed Abdalah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 30. | Government Procurement Services Agency S. L. P 9150, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 4, Kitalu Na. 4, Mtaa wa Bohari Kuu, Eneo la Keko, Temeke, Dar es Salaam | Geraldine Rasheli (Mtanzania) | Leseni ya Uuzaji jumla wa Mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**EWURA**

217361502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mapendekezo ya NEMC muhimu kufanyiwa kazi

**UCHAFUZI** wa hali ya hewa unaosababishwa na moshi wa viwandani na magari mabovu, limekuwa tatizo kubwa duniani na Tanzania ikiwamo.

Tatizo hili linaathiri afya za watu na kusababisha magonjwa yakiwamo ya saratani na serikali kuingia gharama kubwa ya kuagiza dawa.

Katika kongamano la mazingira linalofanyika jijini Dar es Salaam na kukutanisha nchi 10 kutoka Afrika, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limependekeza kuimarishwa kwa usafiri wa umma nchini Tanzania kama ilivyo kwa mabasi ya mwendo wa haraka na kupunguza matumizi ya magari binafsi ikiwa ni mkakati wa kupunguza uchafuzi wa hali ya hewa.

Baraza hilo limesema kuna umuhimu serikali ikaimarisha miundombinu ya usafiri ili wananchi wengi waweze kutembea kwa miguu na baiskeli badala ya kutumia magari.

Tunaungana na NEMC katika mapendekezo hayo, kwa sababu katika baadhi ya nchi zilizoendelea wameweka kipaumbele kwenye matumizi ya baiskeli kama njia ya usafiri badala ya magari ili kupunguza hewa ya ukaa ambayo inachafua mazingira.

Njia zilizopendekezwa ikiwamo watu kutembea kwa miguu husaidia pia kuwaweka katika afya imara na kuwaepusha na magonjwa yasiyoambukiza.

Kuendesha baiskeli na kutembea kwa miguu ni mazoezi mazuri yanayomfanya mtu kuimarika kiafya na kujiepusha kila mara kumuona daktari kwa sababu ya kusumbuliwa na magonjwa.

Nchi zinazowakilishwa kwenye kongamano hilo la siku tatu ni pamoja na Kenya Zambia, Zimbabwe, Ethiopia Uganda Rwanda, Msumbiji, Ghana, Nigeria na Mauritius.

"Tumekutana hapa kubadilishana uzoefu kuhusu kila mmoja anachofanya ili kupunguza uchafuzi wa hali ya hewa kwenye miji yetu kwasababu uchafuzi wa hewa unaathiri sana afya za wakazi wa hiyo miji, kwa hiyo jitihada kama hizi lazima zifanyike." alisema Dk. Samuel Gwamaka, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC.

Kuna visababishi vingi vya uchafuzi wa hali ya hewa kama viwanda kwa kiasi kikubwa, lakini magari hasa yale chakavu ni chanzo kikubwa cha uchafuzi wa hali ya hewa.

Nchi nyingi zinazoendelea kimaendeleo kunasababisha ongezeko kubwa la magari maeneo ya mijini hivyo kuongeza tatizo la uchafuzi wa hali ya hewa.

Kwa mujibu wa NEMC, magari mengi yanayoagizwa ni yale yaliyotumika miaka mingi na kuwa chakavu matokeo yake yanatoa hewa chafu na kuchafua hali ya hewa na mazingira kwa ujumla.

Baraza hilo limeona haja ya kuhamasisha matumizi ya usafiri wa umma kupunguza wingi wa magari barabarani.

Pia, umuhimu wa kujenga barabara zitakazokuwa na maeneo mazuri ya watembea kwa miguu na waendesha baiskeli kama ilivyo kwenye nchi zilizoendelea.

Takwimu zinaonesha namna gani uchafuzi wa hali ya hewa umekuwa chimbuko kubwa la maradhi mengi Afrika na duniani na jitihada zisipochukuliwa afya za watu wengi duniani zitakuwa shakani.

Tanzania uchafuzi wa hali ya hewa ni tatizo ingawa hewa safi kulinganisha na nchi zingine za Afrika, lakini bado kuna mengi ya kufanya kufikia viwango vya Shirika la Afya Duniani (WHO), kuhusu uchafuzi wa hali ya hewa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Taka za sokoni sasa inakaribia kuwa 'dili' la kuinua uchumi kwa jamii

**UNAPOTAJA** soko la kawaida, kwa maana kunakouzwa bidhaa za maisha ya kawaida, hapo unamgusa kila mtu. Ndiko penye mzizi wa vyakula na walaji wanaofika hapo kuvinunua. Muhimu ni kuwa na pesa mfukoni.

Na hayo masoko ndiyo yanaipa miji uhai kwa kukusanya vyakula na hasa mijini na ndio panapofungua uhai wa huduma hizo, huku kukiwa vituo vya kuwezesha biashara kufanyika kwa kina, kuanzia wauzaji, madalali na wanaoleta mizigo kutoka mikoani wanapata mahali pa kufikisha mizigo yao, huku hata picha halisi ya kibiashara katika eneo hilo inakuwa bayana.

Kama kawaida tunaingia katika maisha yanayotukamata 'kizuri hakikosi kasoro'. Kupitia kundi tunaloishi maisha sokoni kuna shida yake kwamba pana kiasi kikubwa cha uzalishaji taka kila kukicha na hilo linatoa maana kubwa katika suala la pa kupatunza.

Ni bahati mbaya katika jamii, wengi tunachukulia suala la uchafu ni zao la kupita halina maana, kumbe linashika maisha yetu ya kila wakati. Hapo ndipo inachukua sura ya kisheria, inazolewa na kuchomwa kufika ngazi ya usafi.

Zipo taka tumekuwa tukiona zinakusanywa 'mitaani' na kulipiwa ushuru kila nyumba, kisha taka hizo zinapelekwa kwenye dampo kwa ajili ya kutupwa. Ukusanyaji taka umekuwa ukifanyika katika mitaa na kupelekwa katika dampo na baadhi ya kampuni zimekuwa zikikusanywa taka ikiwamo magari ya halmashauri.

Somo la kukusanywa taka, ni kuhakikisha mazingira yanakuwa safi na salama.

Ukiangalia kuna taka ambazo zinazalishwa hospitali kwenye vituo vya afya, majumbani na sokoni, huchukuliwa na kupelekwa sehemu kunakostahili.

Baadhi ya jamii nazo hazina elimu sahihi kwamba, taka za majumbani na sokoni zinaweza kuwainua kiuchumi wananchi.Hiyo ni kutokana na kukosa elimu ya kushughulikia taka hizo. Zimekuwa zikichukuliwa majumbani na sokoni na kwenda kutupwa dampo.

Hivi karibuni. Mwenyekiti wa kikundi cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, Selemani Bishagazi, akaja na darasa jipya la umma, kwamba taka za sokoni kwao ni fursa na zitawasaidia watu kuinuka kiuchumi.

Hiyo ni kutokana na baadhi ya jamii kutojua taka za majumbani na sokoni, jamii inaweza kuzigeuza kuwa bidhaa hai na muhimu kwao. Hicho pekee ni kitega uchumi tosha kuhudumia uchumi wetu na kumuingizia kipato mtyu mmoja mmoja, katika maisha ya kila siku.

Kikundi cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Dar es Salaam kinasema kuwa taka ni mali na inaziwezesha jamii kujiongezea kipato kupitia taka hizo.

Kwa mujibu wa mwenyekiti wao, mwana - mazingira Bishagazi, muda sio mrefu wataanza kununua taka za sokoni kwa malighafi ya uzalishaji.

Anasema kupitia hizo taka, anaamini watapata mbolea, vyakula vya kuku na mkaa. Ni maendeleo mazingira ya uchumi zinashikana, ikiwazalishia biashara.

Kazi yao katika hilo, pia watatoa mafunzo kupitia matumizi ya taka hizo, hata kupata manufaa za kutengenezea mbolea,mkaa na chakula cha kuku yanayofanana nayo.

Ni manufaa ya mafunzo, ambayo yanapowapata watu mitaani, inawasaidia kubana matumizi ya pesa, kwa kuwa hawatanunua tena mahitaji kama ya mkaa, pia wanapolima mazao kama mboga wanakuwa na mbolea wanazalisha wenyewe bila ya kupata shida. Wale ambao watafuga kuku, watanufaika kupitia mafunzo hayo wakitengenezea chakula cha kuku.

Anaongeza kuwa ni teknolojia inayopunguzia serikali gharama za kubeba taka kupeleka dampo.

# Wanne mbaroni wizi mabomba ya mradi

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linawashikilia wakazi wanne wa eneo la Kibugumo, Wilaya ya Kigamboni kwa tuhuma za kuiba mabomba ya maji ya mradi wa Kisarawe II unaokwenda Kigamboni.

Mradi huo ni miongoni mwa mikubwa inayotekelezwa na serikali na inasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kusambaza maji kwa wakazi wa Kigamboni.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam Jumanne Muliro, alisema watuhumiwa hao walikamatwa Aprili 8, mwaka huu katika eneo hilo wakiwa na mabomba yenye upana wa inchi sita wakitaka kuyasafirisha na gari lenye namba za usajili T. 719 AGL aina ya Mitsubish Canter.

"Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi limefanikiwa kumkamata dereva wa gari hilo, Emanuel Msofe, mkazi wa Keko Magurumbasi na wenzake watatu wakiwa wanajiandaa kusafirisha mabomba hayo," alibainisha na kuongeza:

"Pia Jeshi la Polisi linaendelea kufanya mahojiano ya kina na watuhumiwa hao, kubaini kabla ya kuwakamata, wameiba mara ngapi na mabomba mangapi yameshaibwa tayari mpaka sasa," alisema Muliro.

Kamanda Muliro aliongeza kuwa ufuatiliaji wa kina unaendelea kufanyika ili kubaini mtandao wa wezi wa vifaa hivyo vya mradi wa maji, na kama kuna watuhumiwa wengine wanahusika kuiba, kuuza au kuuziwa ili sheria ziweze kuchukuliwa haraka.

"Jeshi la Polisi halikubaliani na wizi huu na litafanya kila jitihada, kufuatilia kwa yeyote aliyehusika na wizi huo na hatua kali za kisheria zinachukulia, kuhakikisha kwamba miradi ya serikali haichezewi," alisisitiza Muliro.

**"Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi limefanikiwa kumkamata dereva wa gari hilo, Emanuel Msofe, mkazi wa Keko Magurumbasi na wenzake watatu wakiwa wanajiandaa kusafirisha mabomba hayo," alibainisha na kuongeza:**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo (kushoto), akipanda mti wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Aprili ya kijani iliyoandaliwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Morogoro mwishoni mwa wiki. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# Wataka maboresho mifumo bidhaa zinazouzwa nje

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa kilimo nchini wameishauri serikali kuweka mifumo mizuri itakayodhibiti wauzaji wa mazao nje ya nchi wasiozingatia viwango na ubora wa bidhaa zinazohitajika kimataifa katika kulinda heshima na fursa ya kuuza.

Kauli hiyo imekuja wiki moja tangu Balozi wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki, kukemea tabia ya baadhi ya kampuni zinazouza maharage ya soya katika soko la China kupeleka nafaka hiyo yenye mawe na wadudu hali inayoliharibia taifa sifa.

Akizungumza kupitia mtandao wa kijamii wa tweeter, Mbelwa aliwasihi wafanyabiashara hao kuzingatia masharti ya ubora wa bidhaa zao ili kutoipoteza fursa hiyo muhimu ambayo mataifa mengi yanapambana kuipata.

"Tukiendelea na utaratibu huu wa kuleta vitu ambavyo havikidhi mahitaji ya soko tunajiharibia wenyewe. Kwanza tunaharibu kazi kubwa iliyofanyika kutafuta hili soko na pia tutafanya wanunuzi waamue kununua bidhaa hii kutoka nchi nyingine," alisema Mbelwa.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Kilimo Kusini mwa Afrika (SACAU), Dk. Sinare Yusuph, alisema serikali inapaswa iweke maghala ya kuhifadhia mazao yanayokwenda kuuzwa nje ya nchi, ili yasafishwe na kujiridhisha ubora wake kabla ya kupelekwa katika nchi hizo.

"Bahati yetu mbaya ni kwamba mtu anavuna maharage, anayaweka nyumbani kwake, halafu akipata oda ya kupeleka China ndio anayachukua na kuyapeleka moja kwa moja, hii inatoa mwanya kwa wafanyabiashara kutozingatia ubora unaohitajika," alisema Sinare.

Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Dk. Elly Ligate, alisema kuna umuhimu wa serikali kuanzisha utaratibu wa kuuza mazao hayo kupitia vyama vya msingi vya chakula na kila bidhaa iwekwe stakabadhi yenye jina la muuzaji.

Alisema njia hiyo itawaondolea serikali mzigo wa kudhibiti kwa kuwa kazi hiyo itafanywa na vyama hivyo na ikitokea haina ubora itarudishwa kwa muuzaji kwa kuwa stakabadhi hizo zitaonyesha jina na anwani ya mhusika.

"Kukosa uaminifu na kufanya biashara za kidanganyifu ni moja ya tabia za Watanzania. Sio tu kwenye maharage, wapo wengine wanaweka maji au mawe kwenye mitumba ya tumbaku na pamba, dawa ni kuanzisha uuzaji wa maharage kupitia vyama vya msingi," alisema Dk. Elly.

Mfanyabiashara wa maharage kwa jumla katika soko la Tandika, Shekhe Mbwana, alisema serikali ihakikishe mazao yanayopelekwa nje ya nchi yamezalishwa nchini kwa sababu kuna baadhi ya wafanyabiashara wananunua nchi za jirani na kuzipeleka nje ya nchi hali inayoiharibia jina nchi.

"Kuna baadhi ya wafanyabiashara hasa wa maharage wakiona msimu wa zao hili hapa nchini hakuna, wanakwenda kununua Malawi au Zambia, huko wanapewa yenye wadudu halafu wanapeleka nje ya nchi kwa jina la Tanzania, serikali itupie jicho na hili," alisema Mbwana.

Aidha, alisema tatizo lingine ni kuwapo kwa madalali wanaonunua mazao hayo kwa bei ya chini kutoka kwa kampuni na kuuza nje ya nchi bila kuzingatia ubora.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# China yasema imekuwa wazi utafiti chanzo UVIKO-19

**Na Mwandishi Maalum**

CHINA imesema imekuwa wazi kushiriki matokeo ya utafiti ufuatiliaji wa chanzo cha SARS-CoV-2 na jumuiya ya kimataifa, Shen Hongbing, Naibu Mkuu wa Idara ya Kitaifa ya Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa ya China na Mkurugenzi wa Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa cha China (China CDC) amesema kwenye mkutano na waandishi wa habari, mwishoni mwa wiki.

"Tangu kuzuka kwa UVIKO-19, tumekuwa tukiwasiliana na kushirikiana kikamilifu na Shirika la Afya Duniani (WHO) na kuialika WHO kutuma wataalam wa kimataifa mara mbili kufanya utafiti wa pamoja juu ya ufuatiliaji chanzo cha SARS-CoV-2 nchini China," alisema Shen alipokuwa akielezea juhudi za China katika suala hilo.Kwa mujibu wa Tovuti ya Gazeti la Umma nchini humo, Shen alisema, utafiti wa pamoja wa kipindi cha kwanza ulifanyika kwa mafanikio mjini Wuhan, huku ripoti ya utafiti kuhusu upande wa China ikitambuliwa kikamilifu na wataalamu wa ndani na nje na WHO.

"Katika utafiti wa pamoja wa kipindi cha kwanza, China iliwapatia wataalam wa kimataifa data zote zinazohusiana na chanzo cha virusi na hatukuficha kisa, sampuli au matokeo ya uchunguzi na uchambuzi," alisema.

Akizungumzia kukanushwa kwa matokeo ya utafiti hivi karibuni na maofisa na wataalam fulani wa WHO, Shen alisema hiyo ni kinyume na kanuni za kisayansi na ni tusi kwa wanasayansi hao ambao walishiriki katika kutafuta chanzo.

Aliongeza kuwa, China iliendelea kushiriki kupatikana kwa matokeo ya utafiti na jumuiya ya kimataifa ya wanasayansi baada ya kumalizika kwa utafiti wa pamoja wa kipindi cha kwanza na matokeo yake yaliyochapishwa katika majarida ya kitaaluma ndani na nje ya nchi.

"Tulishiriki pamoja katika kujadili kuhusu data na kufanya uchambuzi na utafiti wa kina wa pamoja na matokeo yalikubaliwa na wataalam wote," Zhou Lei, mtafiti mwenza katika CDC ya China ambaye alishiriki katika utafiti wa pamoja huko Wuhan alisema.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na wenye Mahitaji Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (katikati) akipiga makofi baada ya kuzindua akaunti mpya ya Mwanamke-Hodari ya Benki ya Azania jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Esther Mang'enya na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara ya benki hiyo, Rhimo Nyansaho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Chuo kuongeza uandaaji walimu wa ufundi

**Na Restuta James**

CHUO cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro (MVTCC), 'kinatembea' na kasi ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika kuzalisha walimu wa ufundi stadi kikijipanga kuzalisha wataalam hao 660 kila mwaka.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu mwishoni mwa wiki, Mkuu wa chuo hicho, Samwel Kaali, alisema wameandaa mpango mkakati wa miaka mitano kuanzia mwaka 2023/24 hadi 2027/28, kuhakikisha vyuo vya ufundi vinavyojengwa kila wilaya, vinapata walimu wa ufundi.

Alisema wameandaa mpango mkakati utakaowezesha kutoa walimu 3,100 ndani ya miaka mitano, kukidhi mahitaji ya nchi.

Alisema ili kufanikisha hilo, wameongeza udahili kutoka wanafunzi 120 kwa mwaka hadi 660 na utekelezaji wake utaanza mwaka huu wa fedha.

Alisema wameandaa kozi ya Stashahada ya Uzamili ya Elimu ya Ualimu wa Ufundi na Ufundi Stadi (Post Graduate Diploma in Technical and Vocational Teacher Education), inayotolewa kwa ushirikiano na Chuo Kikuu Huria.

Kaali alisema kuanzia mwaka huu wa fedha, MVTCC inaanzisha stashahada ya walimu wa ufundi na ufundi stadi (diploma in engineering with technical and vocational teacher education).

"Programu tunazoendelea nazo ni cheti cha walimu wasaidizi wa ufundi stadi, stashahada ya walimu wa ufundi na ufundi stadi ambazo ni maalum kwa mafundi ambao wanataka kuwa walimu wa ufundi," alisema.

Kaali alisema tayari chuo kimeandaa mazingira ya kupokea idadi hiyo ya wanafunzi na tayari wameongeza hosteli na vyumba vya madarasa.

"Tunaongeza karakana mbili za ufundi wa uchakataji wa chakula na kozi ya urembeshaji na utiaji nakshi. Tunaenda kukarabati na kuweka vifaa vipya kwenye karakana nne zilizopo, tunatanua maktaba na kujenga kituo cha teknolojia za kidigitali," alisema Kaali.

Alisema mpango wa muda mrefu wa mamlaka ni kujenga chuo kingine cha ualimu wa ufundi stadi kwa kuwa eneo la MVTCC ni dogo.

Mpango huo wa MVTCC unakuja wakati ambao serikali imeanza kujenga vyuo vya ufundi stadi kila wilaya nchini.

Katika mwaka huu wa fedha, Serikali ya Dk. Samia ilitenga Sh. bilioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi huo.

# Uwekaji alama hifadhi Serengeti waungwa mkono

**Na Mwandishi Wetu**

HIFADHI ya Taifa ya Serengeti (SENEPA), imesema kuwa hakuna ardhi ya wananchi inayoporwa katika uwekaji wa alama za mpaka kwa mujibu wa sheria na kwamba mwitikio na ushirikiano wa wananchi wa eneo hilo ni mkubwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana wakati wa uwekaji wa alama hizo katika Kata ya Nyanguru, Mkuu wa Idara ya Ulinzi wa SENEPA, Davis Mushi, alisema uwekaji wa alama ni kutengenisha hifadhi na vijiji vilivyopo kaskazini mwa hifadhi hiyo ili kuondoa migogoro inayoibuka mara kwa mara kwa wananchi kusema hawajui mipaka.

Alisema kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto kutokana na wananchi kutojua eneo la hifadhi hali iliyosababisha changamoto nyingi.

"Hii itasaidia sana kulinda Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na wananchi watakuwa salama, wataondokana na bughudha za kukamatiwa mifugo mara mtu kaingia na hajui kama yupo ndani ya hifadhi, hakuna mpaka mpya unaowekwa bali ni utekelezaji wa GN ya mwaka 1968," alisema.

Mkazi wa Kijiji cha Nyangage, Meshack Mwita, alisema aliwaomba wananchi wenzake kuheshimu mpaka uliowekwa kwa kuwa uko kisheria.

"Tayari tumewekewa alama kuonyesha sisi wananchi tunaishia wapi na hifadhi inaishia wapi, haitakiwi kuvuka kuingia upande mwingine, nawasihi vijana wenzangu watafute kazi maana uwindaji hauna maana tena, unakamatwa unakwenda gerezani miaka mingi unaiacha familia yako inateseka, wakati maliasili hii ingetunzwa ingesaidia vizazi vijavyo," alisema.

Mkazi wa Kijiji cha Msanga, Samweli Chacha, alisema kilichofanywa na serikali ni jambo jema kwa kutambulisha mpaka kisheria ili wananchi watambue mwisho wao ni wapi na kutoingilia wengine.

Kuhusu wananchi waliootesha mazao ndani ya eneo la hifadhi, Mushi alisema; "Walisema hawajui mpaka uko wapi, kwa kuwekwa alama hii wameshajua mpaka, baada ya kuvuna naamini hawataotesha tena.

"Wananchi wengi walikuwa wanatambua mpaka ila hawakuwa wanajua alama iliko. Hili ni zoezi halali hakuna ardhi inayoporwa bali tunaweka alama palepale kwenye GN ya mwaka 1968, tumepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wananchi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Michael Mtenjele, alisema uwekaji alama umeshamalizika kwenye eneo la milima na misitu na sasa wamefika kwenye maeneo ya vijiji.



## Wapatiwa mafunzo ya kwenda kuzifundisha kaya masikini

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WAWEZESHAJI 40 kutoka ngazi ya wilaya wamepatiwa mafunzo yatakayowawezesha kwenda kuzifundisha kaya zilizoko kwenye mpango wa kunusuru umasikini ili ziweze kuunda vikundi vya kujiwekea akiba.

Mradi huo unatekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) awamu ya nne.

Mafunzo hayo ya siku tano yalifunguliwa mwisho mwa wiki na Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru, Elizabeth Ngobei.

Kaimu Mkurugenzi huyo aliwataka wataalamu hao kutumia maarifa watakayopata kuiwezesha jamii katika kujiunga kwenye vikundi ili kujiinua kijamii na kiuchumi.

Alisema watumishi wa serikali wakitumia vizuri fursa hiyo itasaidia kayahizo kujiunga kwenye vikundi pamoja na kuhakikisha vinatekekeza majumu yao kulingana na mpango utaratibu iliowekwa na TASAF.

"Mna jukumu kubwa la kuhakikisha wanakaya hasa kinababa kutambua umuhimu wa kujiunga kwenye vikundi vya huduma ndogo za fedha, na siyo kuwaachia wanawake peke yao, jambo ambalo linaleta mgogoro kwenye kaya kwa kuwa wanaume wanatakiwa kufahamu fedha za TASAF ni za kaya nzima," alisema.

Mratibu wa Huduma za Vikundi TASAF, Ester Kivuyo alisema lengo la mafunzo hayo ni kuzijengea uwezo kaya za walengwa kuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba na kutumia akiba hizo kukopeshana katika vikundi.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Arusha, Grace Makema, alisema lengo la mafunzo kwa watalamu hao ni kuwajengea uwezo watakaokwenda kuzifundisha kaya ngazi ya kijiji.

Alisema wawezeshaji hao watakwenda kuwafundisha wanakaya namna ya kuanzisha, kusajili vikundi.

Alisema pia watawafundisha kuhusu uongozi wa vikundi, uandaaji wa katiba, elimu mwendo kwa vikundi, kuweka akiba, kuwekeza,usimamizi wa mikopo, utunzaji wa kumbukumbu na urejeshaji wa mikopo.

# Kibong'oto yaibuka kidedea utoaji wa matibabu ya TB

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

HOSPITALI Maalum ya Rufani ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto, imekuwa kinara wa utoaji wa mafunzo na matibabu ya magonjwa ya kifua kikuu sugu kwa njia ya mtandao wa masafa nchini.

Katika utoaji wa mafunzo na matibabu hayo zaidi ya wagonjwa 160 wamefikiwa na huduma hiyo kwa njia ya mtandao wa masafa, huku watoa huduma zaidi ya 600 wakifaidika na mafunzo hayo yaliyoanzishwa mwaka 2017.

Hayo yalisemwa jijini Arusha mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk.Leonard Subi, wakati akitoa mafunzo ya uboreshaji wa mtaala wa njia ya masafa ya kifua kikuu sugu kwa waratibu wa kifua kikuu wa kanda kwa baadhi ya mikoa na halmashauri nchini.

Alisema lengo la utoaji wa mafunzo hayo ni kuimarisha matibabu na kudhibiti ugonjwa wa kifua kikuu sugu.

Hata hivyo alisema awali kulikuwa na matatizo ya kuhudumia wagonjwa wengi katika hospitali hiyo lakini baada ya kuanzisha utoaji wa mafunzo na matibabu ya magonjwa hayo kwa njia ya masafa imesaidia huduma hiyo kufika maeneo mbalimbali nchini kwa wakati.

"Zaidi ya asilimia 75 ya wagonjwa wa kifua kikuu sugu wamekuwa wakipona endapo wakifuata ushauri wa madaktari ikiwamo kutumia dawa na tumekuwa tukisisitiza kila mgonjwa apime makohozi.

"Serikali chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imenunua na kusambaza mashine za Gene Expert zaidi ya 350 kwenye halmashauri na hospitali mbalimbali nchini za kupimia makohozi na zinatoa majibu baada ya saa mawili tofauti na huko nyuma mgonjwa alikuwa anasubiri majibu kwa siku tatu,"Dk. Subi.

Aidha, alisema ugunduzi wa magonjwa hayo bado uko chini kwa kuwa wamekuwa wakigundua wagonjwa hao kwa asilimia 65 tu jambo ambalo linachelewesha udhibiti wa mnyororo wa maambukizi ya TB nchini.

Vilevile alitoa rai kwa jamii wanapona dalili za ugonjwa ikiwamo kukoa kwa wiki mbili au zaidi, homa hasa nyakati za jioni, kutoka jasho wakati wa usiku, kupungua uzito na hata kukoa makohozi yaliyochanganyika na damu wafike vituo vya huduma kwa uchunguzi na matibabu.

Mtaalamu Mshauri wa Kifua Kikuu Sugu kutoka hospitali hiyo, Dk.Peter Daud, alisema mafunzo kwa njia ya masafa yalianza baada ya kuwepo kwa matatizo kwa wagonjwa sugu wa kifua kikuu kutoka maeneo mbalimbali.

Mtaalamu wa Sayansi za Maabara kutoka Shirika la MDH, Magreth Antony, alisema lengo la kuwakutanisha watoa huduma hao ni kuwezesha kuandaa mtaala wa kufundishia wataalamu mbalimbali wa kada za afya namna ya kutambua magonjwa ya TB, kuwahudumia kwa kutumia dawa na miongozo ambayo ipo kitaifa.

Kadhalika alisema mafunzo hayo huwa yanafanyika kwa njia ya masafa na kwa sasa yanatolewa na vituo viwili ambavyo ni Hospitali ya Kibong'oto na Hospitali ya Benjamini Mkapa iliyoko mkoani Dodoma.

Aidha, alitoa wito kwa wataalamu wa kada za afya kujiunga na mafunzo hayo ili kuongeza uelewa zaidi katika utoaji wa huduma hizo.



Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mchengerwa (katikati) akimfungulia mlango wa gari, Shamimu Mushi (kushoto), aliyejishindia gari mpya kupitia promosheni ya Kapu la Wana inayoendeshwa na kampuni ya bia ya Serengeti (SBL), kupitia bia yake ya Pilsner Lager, jijini Arusha mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meneja Mauzo wa SBL Kanda ya Kaskazini, Andrew Msiagi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC ahimiza vikundi vilivyopata mikopo kufanya marejesho

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKUU wa Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, Emmanuela Kaganda, ameviagiza vikundi vya wanawake na vijana waliopatiwa mikopo na Halmashauri ya Arusha, kurejesha fedha hizo kwa wakati ili ziweze kuwanufaisha watu wengine.

Alitoa agizo hilo jana wakati wa hafla ya kukabidhi mkopo wa Sh.milioni 274 kwa vikundi 37 vya wanawake na vijana katika halmashauri hiyo.

Aidha aliwasisitiza wanavikundi hao kutambua kuwa fedha hizo zinatakiwa kurejeshwa baada ya kipindi cha neema kupita, hivyo ni vyema kuzitumia kwa kufanya miradi waliyoiandika kwenye maandiko yao na kuzirejesha kwa wakati.

"Tukirejesha fedha hizi kwa wakati kutatoa fursa ya kuwakopesha wengine na sisi wenyewe kukopeshwa kwa awamu nyingine, tumieni fedha hizi kwa nidhamu,"alisema.

Pia aliwataka wanawake kuwahamasisha na kuwaelimsiha vijana ili waweze kunufaika na mikopo isiyo na riba inayotolewa na serikali kupitia asilimi 10 za mapato ya ndani ya halmashauri.

Aidha, wanavikundi waliopokea mikopo hiyo waliishukuru serikali kwa kuwapa fedha zitakazowasaidia kujikwamua kiuchumi.


Habibu Malia, kijana mwenye ulemavu aliishukuru serikali kwa mpango huo akisema utawasaidia wananchi kujikwamua kiuchumi.

Joseph Mibaroi kutoka kikundi cha Kidali Youth cha Kata ya Mwandeti alisema: "Tunaishukuru serikali kwa kutupa mikopo hii yenye masharti nafuu, sisi vijana wa kijijini tumeweza kukopesheka, jambo ambalo halipatikani kwenye taasisi nyingine za kifedha".

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, alisema kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu halmashauri hiyo imefanikiwa kutoa mikopo ya Sh.bilioni 1.3 na kwa kipindi cha miezi sita ya mwaka wa fedha 2022/23 imekopesha Sh.milioni 509.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Arumeru, Noel Severe, alipongeza halmashauri kwa kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya kupambana na umaskini kwa kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapa mikopo hiyo.

Alisema: "Mikopo hii ni utekelezaji wa ilani ya CCM, hivyo mnapaswa kuhakikisha mnaitumia vizuri iweze kuinua vipato vya familia pia tunategemea mkapambane na kuirejesha kwa wakati kulingana na utaratibu".



# Wakulima tumbaku, pamba wakumbushwa kuweka akiba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Mkoa wa Kahama, umewakumbusha wakulima wa tumbaku na pamba kujiwekea akiba katika mfuko huo kupitia sehemu ya fedha wanazozipata kila msimu wa kilimo ili kujikwamua kimaisha.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Kaimu Meneja wa NSSF, Shabani Mbwana wakati akizungumza na wakulima wa zao hilo katika Kata ya Bukomela na Uyogo Halmashauri ya Msalala kutoka vyama vya msingi 10 vya Mliza, Ngokolo, Kabila, Ibalagalimi, Isebamabega, Kabila, Uyogo, Mshikamano, Manungu na Kazena.

Alisema kila mkulima wa mazao ya chakula na biashara anawajibu wa kujiwekea akiba kupitia mfuko huo kuanzia Sh.20,000 kila mwezi kupitia fedha anazozipata baada ya kuivisha mazao na atakayechangia ipasavyo atakuwa na sifa ya kupata pesheni na zitakazomsaidia pale atakapokosa nguvu ya kulima.

Aidha, alisema miongoni mwa faida za kuwekeza ni pamoja na mwanachama mwanamke atapata fao la uzazi na anatakiwa kuchangia angalau miezi 36, ambapo miezi 12 iwe karibu na muda wa kujifungua.

Alisema pia awe anategemea kujifungua au ameshajifungua mtoto atalipwa baada ya miaka mitatu isipokuwa ikiwa mtoto amefariki ndani ya miezi 12 baada ya kuzaliwa.

Mmoja wa wakulima kutoka Chama cha Msingi Ngokolo, Daniel Bandika alisema alikuwa hafahamu kama wakulima nao wanaweza kujiwekea akiba kupitia NSSF na badala yake alikuwa anafahamu wanaoweka akiba ni wafanyakazi waliojiriwa na serikali na taasisi binafasi.

Alisema kwa kuwa bado ana nguvu na uwezo wa kuzalisha mazao ya chakula na biashara yuko tayari kujiunga na NSSF na kuchangia michango kila mwezi na atahakikisha familia yake yote inakuwa mwanachama ili pale watakapokosa nguvu ya kuzalisha basi wawe wameshapata sifa ya kupata fao la uzeeni.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Hamisi Majogolo alilitaka shirika hilo kuhakikisha linawafikia wakulima wote katika Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama na kuwapatia elimu ya umuhimu wa kujinga na mfuko huo na kuwaondoa dhana ya kuwa NSSF ni kwa ajili ya wafanyakazi tu.



Maofisa Mazingira kutoka Geita, wakiwa na viongozi mbalimbali wakikagua namna wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu Geita Resources katika Machimbo ya Nyamatagata, walivyotunza mazingira kwa kupanda miti hekta 2000 katika eneo ambalo wamemalizia kufanya shughuli za uchimbaji katika Halmashauri ya Geita Mji hivi karibuni. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wachimbaji madini wapanda miti kudhibiti mmomonyoko

**Na Marco Maduhu,** GEITA

WACHIMBAJI wa wadogo wa madini ya dhahabu Geita Resources wamepanda miti ili kudhibiti mmomonyoko wa udongo pamoja na uharibifu wa mazingira katika eneo la machimbo ya madini Nyamtagata lililopo Halmashauri ya Mji wa Geita.

Mkurugenzi Msaidizi wa Geita Resources ambaye pia ni mtaalamu wa mazingira, Yusuph Kulwa, alibainisha hayo juzi wakati maofisa mazingira kutoka mkoani Geita pamoja na timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa vitendo (LEAT) walipotembelea mgodi huo kuona namna wanavyotunza mazingira.

Alisema uchimbaji wa madini katika machimbo ulianza mwaka jana na kulikuwa na watu takribani elfu 20 hali iliyosababisha uharibifu mkubwa wa mazingira, hivyo kuwafanya wao kama sehemu ya wamiliki wa leseni katika eneo hilo kuanzisha shughuli za upandaji miti ili kudhibiti hali hiyo.

"Watu walichimba sana madini na uharibifu wa mazingira ulikuwa mkubwa, lakini baada ya madini kuisha eneo hili tutaona si vyema kuliacha hivyo hivyo bali tufukie mashimo na kupanda miti," alisema Yusuph.

Aidha, alieleza kuwa tayari wamezalisha vitalu vya miche ili kila eneo ambalo watamaliza uchimbaji katika machimbo hayo watarudishia mashimo na kupanda miti, lengo ni kuzuia uharibifu wa mazingira na kurudisha uoto wa asili,"aliongeza.

Ofisa Mazingira Mkoa wa Geita, Tito Mlelwa, alisema kitendo walichokifanya wachimbaji hao wa wadogo katika machimbo ya Nyamatagata, kinafaa kuigwa na wachimbaji wengine kote nchini ili isionekane wachimbaji wadogo ni waharibifu wa mazingira, bali ni watunzaji wazuri pia wa mazingira.

Naye Valeria Macha kutoka LEAT alisema wamekuwa wakitoa mafunzo kwa viongozi mbalimbali pamoja na wachimbaji wa wadogo kufanya uchimbaji wa madini bila ya uharibifu wa mazingira na kupongeza machimbo hayo ya Nyamatagata kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira.

# CCM Tarime watakiwa kumaliza tofauti zao

**Na Timothy Itembe,** MARA

MJUMBE wa Mkutano Mkuu Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chonchoria amewataka wajumbe wa chama hicho wilayani Tarime kumaliza tofauti walizonazo na kuanza shughuli za kukijenga chama pamoja na kutatutua changamoto za wananchi.

Inaelezwa kuwa baada ya uchaguzi wa ndani wa chama hicho wanachama waligawanyika na kuwa na migogoro ya mara kwa mara hali inayodhohofisha chama hicho pamoja na maendeleo ya wananchi ndani ya wilaya hiyo.

Chonchoria alitoa rai hiyo hiyo juzi wakati wa chakula cha pamoja na wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho wilayani Tarime na kuwataka waungane pamoja katika kuhakikisha wanapambana na maadui watatu ujinga, umasikini na maradhi.

Kadhalika, alidai kuwa siasa siyo uadui bali ni umoja, mshikamano na upendo katika kuhakikisha wanabaini matatizo ya wananchi na kuyafanyia kazi kwa haki ikiwa ndilo lengo na hitaji la ilani ya chama hicho.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Tarime, Simioni Kiles aliwataka baadhi ya viongozi katika chama hicho kuhakikisha wanashiriki katika shughuli za kijamii ikiwa ni pamoja na kushiriki katika ujenzi wa shule na mambo mengine yanayokuwa yakihitaji usaidizi wao.

Alieleza kuwa halmashauri itaendelea kutoa fedha inayopatikana na chanzo cha Mgodi wa North Mara katika kuboresha huduma za afya na kupunguza uhaba uliopo wa dawa katika Hospitali ya Bomani inayomilikiwa na Halmashauri ya Mji wa Tarime.

Diwani wa Kata ya Ganyange, Siza Kiheta alisema wapo tayari kuhimiza uchangiji wa ujenzi wa madarasa kata hiyo, huku akitoa Sh.milioni 1.3.

**Chonchoria alitoa rai hiyo hiyo juzi wakati wa chakula cha pamoja na wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho wilayani Tarime na kuwataka waungane pamoja katika kuhakikisha wanapambana na maadui watatu ujinga, umasikini na maradhi.**



Ukurasa 13

Wadau wa elimu wakusanyika kutafakari kuongezea uwezo HESLB

Nipashe
# TESA
Jumanne Aprili 11, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

## Taasisi ya Ustawi wa Jamii yawafunda sumu ya pombe, 'unga' kwao na abiria

ELIMU

NA NEEMA HUSSEIN, MPANDA

# Kundi wanaofeli kidato cha pili Katavi wanakimbia kurudia wakikwepa aibu

• Wakuu shule wabuni staili yao kuwarejesha

KUNA misemo waliitumia sana wazee zamani na inadumu mpaka sasa. Hapo lengo ni kuhamasisha elimu na umuhimu wa mtoto kwenda shule. Hapo kuna 'elimu ni ufunguo wa maisha' na 'mshike sana elimu, usimuache aenda zake".

Hivi sasa serikali imeongeza nguvu kuhakikisha inaboresha miundombinu ya elimu, ikiwamo madarasa, madawati, pia inaboresha mitaala na stadi za kuhakikisha mwanafunzi anaelewa darasani.

Mfano mmojawapo ni kuhakikisha mwanafunzi anayeanza darasa la awali anamaliza darasa la saba bila kikwazo na anayefaulu kwenda kidato cha kwanza, anamaliza kidato cha nne.

Kufanikisha hilo ni mtihani mkubwa. Hapo serikali inaendesha msako wa 'nyumba kwa nyumba' kuhakikisha kila anyestahili kuitwa mwanafunzi anakuwa darasani, ikiwamo ngazi ya wanaonza kidato cha kwanza.

Wakati kuna ishara ya mafanikio, sura ya pili ya changamoto sasa inashuhudiwa, kwa wanaofeli mtihani wa kidato cha pili, hawaendelei na masomo, na ikiangaliwa mahsusi wilayani Mpanda na mkoa Katavi kwa ujumla, linaangukia hatari kubwa kupoteza ndoto zao za baadaye.



Wanafunzi wa kidato cha pili wakiwa darasani, Manispaa ya Mpanda. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

### HALI INAYOENDELEA

Utafiti wa Nipashe umebaini watoto wengi wanaofeli kidato cha pili wanagoma kurudia darasani, kutokana na sababu mbalimbali, baadhi ni za wazazi, pia wanafunzi wenyewe.

Zao lake wanaishia kuzagaa mtaani, mabinti wakiangukia hatari kubwa za kupata ujauzito na kufanyiwa ukatili, hata wakazidi kuzalisha mimba nyingi za utotoni, kwa kukosa mbadala wa kuwa shuleni.

Dk. Baganda Elpidius, ni Ofisa Elimu Mkoa wa Katavi, anasema kisheria endapo mwanafunzi anakosa sifa ya kuendelea kidato cha tatu, anatakiwa arudie ule mtihani katika darasa alilokuwa anasoma.

Anasema endapo mwanafunzi atataka abadilishe shule wao wako tayari kumuhamisha ili akaendelee na masomo katika shule anayotaka kwenda.

"Kuteleza sio kuanguka kukosa mtihani mara moja haina maana kwamba wewe hauna akili yawezekana ni sababu nyingi zimechangia ikiwemo za kimazingira kwahiyo tunatoa wito kwa wazazi, walezi, viongozi, maofisa elimu na halmashauri zote kuhakikisha kwamba wanafunzi ambao hawakufaulu mtihani warejee shuleni warudie kidato cha pili," anasema Dk. Baganda.

"Kuna wanafunzi ambao walisimama masomo kwa sababu za ugonjwa, ugomvi wa wazazi kupata mimba, bado Waraka Namba Mbili wa Mwaka 2021 upo unasema, wanafunzi wa aina hiyo wanarejeshwa shuleni anatamka Dk. Baganda.

### WAKUU WA SHULE

Joseph Tongolo, Mkuu wa Shule ya Sekondari Mwangaza, mjini hapa anasema katika shule yake wanafunzi waliofanya mtihani kidato ni 254 na waliofeli wako 27, kwa maana ya daraja sifuri.

Anasema hao kisheria wanaruhusiwa kurudi kuendelea na masomo, lakini mpaka kufikia Febuari mwanzoni alikuwa amepokea mmoja pekee.

"Wengine ambao hawajarudi wazazi wamekua wakija na kueleza jinsi watoto wao wanavyo fikiria namna ya kurudi kwenye shule walizokuwa wanasoma na tumekuwa tukitoa ushauri, kama anashindwa kurudi shuleni, tunaruhusu atafute shule nyingine anayoona atakuwa huru kusoma bila ya aibu yeyote.

"Kwa hiyo, wapo wanaohama kuelekea shule zingine na sisi pia tunapokea waliofeli kutoka shule zingine. Mimi nashauri tu, hili lingekuwa linawekwa vizuri, kwamba mtoto asijisikie vibaya sana anaporudi kusoma na aliyowaacha kidato cha kwanza," anasema na kudokeza wanawapatiwa elimu mapema ya kurudia darasa, iwapo hawajafikisha wastani.

"Wakifeli, wale majasiri ndio wanarudi, wanakubali wamefeli, wanajipanga upya na wanaendelea na masomo. Tunawapa mfano wa waliofeli na wakarudia na leo wapo nyadhifa mbalimbali wanafanya kazi huko.Wengine ni walimu, wengine ni manesi na kuendelea...

"Wazazi wenye watoto ambao wamefeli kidato cha pili, wafike kwenye shule zao washauriane na walimu, anaweza kuja na mtoto ili ajengwe kisaikolojia na arudi kusoma," anasema Tongolo.

Ni hoja inayoendelezwa na Mkuu wa Shule ya Sekondari Mpanda Day, Patrick Chalamila, anayesema wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha pili katika shule hiyo ni 197 na walioshindwa kuendelea kidato cha tatu ni 59, lakini kati yao waliorudi kuendelea na masomo ni wanafunzi 28, watano wamehamia shule nyingine.

"Baadhi wamechelewa kuripoti shuleni kwa sababu ya kuona aibu, pamoja na sababu zingine lakini sababu kubwa ni kuona

INAENDELEA UK.14

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

DARASA LAO WAENDESHA BODABODA...

# Taasisi ya Ustawi wa Jamii yawafunda sumu ya pombe, 'unga' kwao na abiria

MADEREVA wa bodaboda, ni miongoni mwa watu wanaofanya kazi karibu zaidi na jamii, kwa kutoa huduma ya usafiri. Hata hivyo, baadhi yao wako lawamani wakituhumiwa kujihusisha na uhalifu, hata kuonekana hawafai ndani ya jamii inayowazunguka.

Taasisi ya Utawi wa Jamii imeamua kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo kutambua madhara ya ukatili wa kijinsia, matumizi ya dawa za kulevya na hata msongo wa mawazo, viongozi 50 wa madereva wa bodaboda wa wilaya Kinondoni, Dar es Salaam.

Ni mafunzo yaliyotolewa makao makuu ya taasisi hiyo, Kijitonyama wiki iliyopita, huku Mhadhiri na Mratibu wa Kitengo cha Ushiriki wa Jamii wa Taasisi hiyo, Dunstan Haule, akivifafanua vitendo hivyo ni uhalifu unaochangiwa na matumizi ya pombe na dawa za kulevya.

Anasema, mtumiaji ama pombe au dawa za kulevya, anaweza kujikuta katika matatizo ya kiafya, kisaikolojia, kiuchumi, kijamii, kimazingira na kiusalama na hadi sasa kuna madereva wengi wa bodaboda wanatuhumiwa kwa ukatili wa kijinsia, ikiwamo mimba za wanafunzi, na mara nyingi wanaofanya hivyo ni wanaotumia vilevi.

"Ni muhimu mjue kuwa dawa za kulevya ni kemikali ambazo mtu akizitumia huathiri mfumo wa fahamu na kuleta mabadiliko katika hisia, fikra na tabia na kujikuta hata akifanya mambo asiyoyatarajia," anasema.

### MAANA YA MSONGO

Mratibu wa Kituo cha Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia wa taasisi hiyo, Rufina Khumbe, anawafafanulia kwamba mlevi wa pombe na dawa za kulevya, anavyokuwa, akinena:"Kwanza muhimu muelewe kuwa msongo wa mawazo, ni mfadhaiko wa akili anaoupata mtu kutokana na changamoto mbalimbali katika maisha ya kila siku na kukosa namna bora ya kukabiliana au kutatua changamoto inayomkabili."

Anafafanua kuwa vyanzo vya msongo wa mawazo, ni mazingira ya kazi, uwezo wa kiuchumi, mahusiano, matendo ya ukatili na changamoto za kifedha, mikopo, kufilisiwa, huku dalili zake zikiwa ni mabadiliko katika tabia ya kula, kutopenda kushirikiana na wengine.



Mhadhiri na Mratibu wa Kitengo cha Ushiriki wa Jamii wa taasisi hiyo, Dunstan Haule, akiendesha mafunzo kwa viongozi wa madereva wa bodaboda. **PICHA: SABATO KASIKA**

> Ni muhimu mjue kuwa dawa za kulevya ni kemikali ambazo mtu akizitumia huathiri mfumo wa fahamu na kuleta mabadiliko katika hisia, fikra na tabia na kujikuta hata akifanya mambo asiyoyatarajia.

"Mtu mwenye msongo wa mawazo anakuwa na hasira, anazungumza kwa sauti kubwa, anapoteza hamu ya tendo la ndoa, kuumwa kichwa, kubanwa na misuli, kifua na matatizo ya uyeyushaji wa chakula tumboni," anasema.

Rufina anasema mtu aina hiyo anakuwa na matatizo ambayo hayaponi kwa kutumia dawa, hapati usingizi au kulala sana, anafanya makosa ya mara nyingi katika utendaji kazi, hufanya maamuzi hatarishi na anapoteza kumbukumbu na kuwa na fikra za kujidhuru au kujiua.

"Njia sahihi ya kukabiliana na msongo wa mawazo ni, kutambua chanzo cha msongo, kuwa na mtazamo chanya, kuepuka tabia hatarishi, kuchangamana na watu, kuzingatia muda, kuzungumza na watu unaowaamini na kutembelea Kituo na Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia," anasema.

Anasema kwa madereva, wanaogtumikia jamii, hawana budi kuyaelewa hayo na kuzingatia elimu waliopata, ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi bila kuleta madhara kwa wengine na hata kwao wenyewe.

### AINA YA DAWA HIZO

Mhadhiri Haule anazitaja kitaalamu kuwa ni vileta njozi (hallucinogens) vikimsababishia mtumiaji ahisi kuwa anaona au kusikia vitu visivyokuwapo au tofauti na uhalisia, mfano wake ni utumiaji bhangi.

"Vilevile, kuna vichangamsha mwili, ambavyo huongeza kasi ya utendaji wa mfumo wa fahamu na kuongeza mapigo ya moyo, kasi ya kupumua na uchaji wa akili, kwa mfano cocaine, mirungi na dawa jamii ya 'amphetamine'..." anasema.

Anataja dawa nyinginezo ni vipumbaza mwili, vinavyopunguza kasi ya utendaji wa mfumo fahamu na kushusha mapigo ya moyo, hata akili, akitoa mfano wa dawa za heroin na valium.

Haule anasema, inapotokea mtu akitumia dawa za kulevya, inamuingia kwenye damu, huenda katika sehemu ya ubongo anayoitaja kwa jina 'limbic system' na kwamba ni sehemu inayohusika na kuleta raha ya mwili.

Anajumuisha kuwa dawa za kulevya zikishafika kwenye ubongo, husababisha kutolewa kwa wingi kemikali iitwayo 'dopamine' na kwamba kemikali hiyo ndiyo inayohusika kuleta raha na mtumiaji anapoipata raha hiyo 'isiyo na kifani' inamfanya aendelee kuitumia.

### KWANINI MATUMZI?

Mtaalamu huyo anataja sababu mojawapo ni msukumo rika, migogoro ya kifamilia, kukosa malezi bora, uelewa mdogo wa stadi za maisha, kukosa kazi, kutokujua madhara yake, kujaribu na upatikanaji kirahisi.

"Sababu nyingine ni utandawazi, kibaiolojia, imani potofu kwa kazi ngumu kama za uvuvi, ujenzi, kubeba mizigo, ukahaba kwa kudhani kwamba mtu akitumia anakosa aibu ya kufanya kazi yoyote," anasema.

Anaongeza kuwa kuna njia ya kuwatambua watumiaji wa dawa za kulevya ikiwamo mabadiliko ya tabia, kujihusisha na marafiki wapya ambao, anajitenga na kuwa msiri na hata kubadilika na kuwa mwenye hasira.

"Watu wa aina hii malengo yao hubadilika ghafla, nao hubadilika mwonekano, uchafu, sura, kuwa na tabia ya udokozi, kuuza vitu vyao, madeni mengi, kukosa hamu ya kula au kula sana, kubadilika kwa sauti, kupata ajali za mara kwa mara na kufanya jambo bila ya kutafakari athari zake," anasema.

Mhadhiri huyo anawataka viongozi wa madereva hao, kutambua hayo yote na kuwasaidia wenzao kuachana na tabia, inayoweza kuwaingiza katika vitengo vya uhalifu au kuwasababishia ajali za kila mara wawapo barabarani.

### MADHARA YA UKATILI

Mratibu wa Dawati la Jinsia wa taasisi hiyo, Elizabeth Mashishanga, anayataja ni mazingira yanayorahisisha ukatili wa kijinsia kama kifo, kujiua, mauaji, majeraha na ulemavu.

Anawapa mbinu ya jinsi ya kupinga ukatili wa kijinsia kuwa ni kuzijua sheria mbalimbali, zikiwamo za usawa wa kijinsia na haki za binadamu, kanuni za makosa ya jinai, sheria ya makosa ya kimapenzi, sheria ya watoto, sheria haki na fursa sawa na sheria ya ulinzi dhidi ya ukatili wa majumbani.

Hapo anawataka madereva kuvunja ukimya katika kuzuia ukatili wa kijinsia kwenye shughuli zao na kuwa mfano wa kuigwa katika kumlinda kila mwananchi, kufikisha taarifa katika dawati la jinsia polisi kila inapobobidiau penye vituo vya msaada wa kisaikolojia.

Anafafanua kuwa taasisi hiyo imeanza na viongozi wa madereva wa bodaboda wa wilaya ya Kinondoni, kisha itaenda a wilaya nyinginezo za mkoa wa Dar es Salaam.

Mwakilishi wa madereva hao, Adili Stephen, anakiri mambo mengi hawakuyajua, hasa tafsiri ya kina madhara ya kutumia pombe na dawa za kulevya.

Kiongozi huyo anaiomba taasisi hiyo kuwapa vitambulisho vya kuwatambua, ili waweze kwenda vijiweni kutoa elimu kwa wenzao na jamii, kutafuta matokeo chanya.

ELIMU

NA PAUL MABEJA,
DODOMA

# Wadau wa elimu ya juu wakusanyika kutafakari kuongezea uwezo HESLB

• Ilianza kuhudumia 20,000 sasa wako 70,000

MIGOMO na maandamano kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini miaka ya nyuma lilikuwa jambo la kawaida mithili ya utamaduni wa wanafunzi. Hiyo ni kutokana na madai ya wanafunzi kucheleweshwa malipo kwa wakati.

Ilikuwa staili ya kawaida ya wanafunzi hasa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakati huo kilipokuwa chuo kikuu pekee nchini, wakishinikiza malipo ya madai yao, hasa kwa kiasi kikubwa kabla ya kuanzishwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Miaka ya hivi karibuni, inashuhudiwa migomo kwa wanafunzi wa elimu ya juu imepungua sana kutokana na (HESLB) kuchukua nafasi yake.

Pamoja na mafanikio hayo yanayotajwa, bado bodi hiyo inatajwa inatafuta mikakati mbalimbali ya kupata vyanzo mbadala ili kusadia kumudu kuhudumia kundi kubwa la wanafunzi linaloongezeka kila siku nchini.

Ni zao la ongezeko kubwa la vijana wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu nchini serikali kwa kushirikina na wadau wengine, sasa inaanza mikakati ya kutafuta vyanzo vipya vya mapato vitakavyowezesha wanafunzi wote wanaostahili kupata fedha kwa ajili ya kujiunga na masomo.

Vyanzo hivyo vinatarajiwa kuondoa kero iliyopo sasa ya kutegemea chanzo kimoja cha HESLB, ambacho sasa kinaelemewa na ongezeko la wanafunzi wenye uhitaji.



Wanafunzi wa elimu ya juu katika moja ya nyendo za kushinikiza kupatiwa fedha za mikopo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Abdul-Razaq Badru. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

#### SAUTI YA SERIKALI

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dk.Franklin Rwezimula, anabainisha hayokatika mkutano wa kujadili namna ya kupata vyanzo vipya vya mapato vitakavyo tumika kuhudumia wanafunzi wa elimu ya juu nchini.

Ni hatua inayofikiwa huku kukiwapo uamuzi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akitaka wote wanaochaguliwa kujiunga na elimu ya juu nchini kwa ngazi ya shahada wapate mikopo na stahiki zao.

Dk. Rwezumula anasema, kutokana na mageuzi makubwa ambayo serikali imeyafanya hivi sasa kumekuwepo na ongezeko kubwa na wanafunzi wenye sifa za kujiunga na masomo ya elimu ya juu.

"Chanzo ambacho tunakitegemea hivi sasa ni Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu pekee yake, ambayo hivi sasa haikidhi mahitaji hivyo tumeamua kukutana na wadau kutoka sekta mbalimbali, ili kujadili kwa pamoja na kupata vyanzo vipya ambavyo vitasaidia kusomesha watoto wetu wasiokuwa na uwezo," anasema

Aidha, anasema kikao hicho ambacho kinahusisha wadau mbalimbali kutoka taasisi za fedha, vyuo vikuu, wizara mbalimbali pamoja na HESLB, wanajadili namna bora ya kupata vyanzo hivyo vipya na kuja na maazimio yatakayotoa mwelekeo wa kupata fedha ambazo zitatumika kuhudumia wenye uhitaji.

"Sasa hivi tumepata benki ya NMB, ambao tayari wameshatenga Sh. bilioni 200 ambayo watu wataweza kukopa kwa ajili ya ya elimu ya juu na riba yao ni asilimia tisa. Kwa hiyo, bado tunahitaji kupata wadau wengine watakaohudumia watoto wengi katika vyuo vyetu,"anasisitiza Dk.Rwezimula

Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB). Prof. Mohammed Hafidh, Khalifa, anasema uwekezaji katika sekta ya elimu nchini ni jambo la muhimu na hivi sasa kunawatoto wengi nchini wanaohitaji kupata mikopo, lakini vyanzo vinavyotegemewa ni bodi za mikopo ya elimu ya juu vya Zanzibar na Tanzania Bara.

> Mkutano wetu huu leo utatusaidi kupata namna bora ya kupata vyanzo vipya vya mapato ili kila mtoto anayestahili kujiunga na masomo ya elimu ya juu ajiunge bila kuwapo na kikwazo chochote.

"Mkutano wetu huu leo utatusaidi kupata namna bora ya kupata vyanzo vipya vya mapato ili kila mtoto anayestahili kujiunga na masomo ya elimu ya juu ajiunge bila kuwapo na kikwazo chochote," anasema Prof. Khalifa

Mwenyekiti wa HESLB, Prof. Hamis Dihenga, anasema vijana wanaohitaji mikopo wamekuwa wakiongezeka mwaka hadi mwaka hivyo hawawezi kuendelea kutegenea chanzo kimoja.

"Lengo letu kupitia mkutano huu ni kupata vyanzo vipya vya mapato hatuwezi kuendelea kutegemea serikali pekee yake kwakua ina mambo mengi bado zipo changamoto nyingi na idadi ya wanafunzi wenye sifa ya kupata mikopo inaongezeka kila mwaka, hivyo ni lazima tujadiliane ili kutoka na majibu ya kuwa na vyanzo vipya vya mapato," anasema

Anasema tangu kuanzishwa bodi hiyo mwaka 2005, wanafunzi walippata mikopo walikuwa ni 20,000 na hadi kufikia sasa kuna wanafuzi 70,000 wanufaika wa mikopo hiyo.

#### MKUU WA HESLB

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abul-Razaq Badru, katika kikao hicho na wadau, anasema: "Tathimini ya kwanza ni kuangalia sisi kama serikali wale tunaopita kusoma shahada wanazozisoma zinaendana na soko la ajira.

"Tathimini nyingine ni kuangalia namna gani ya kupata vyanzo vipya kwa ajili ya kulipia watoto,"anatamka.

Kuhusu urejeshaji mikopo, anasema hivi sasa kwa mwaka kiasi cha Sh. milioni 180 kinarejeshwa, illinganishwa naa Sh.miloni 30 za kipindi cha nyuma. Tangu kuanzishwa bodi hiyo, imesharejeshwa Sh. trioni 1.5.

Ongezeko la wanafunzi wa elimu ya juu wanaopata mikopo nchini imechangiwa na sababu kadhaa. Moja ni Mpango wa Kupanua Vyuo Vikuu nchini, kupanua ukubwa wa chuo kikuu kilichokuwapo UDSM na kuanzishwa vipya, kama vile Chuo Kikuu Huria (OUT) na Taasisi ya Uongozi Mzumbe (IDM) kuwa chuo kikuu. Ni hatia iliyoendana na kuzaliwa HESLB.

Hali kadhalika, ni wakati vyuo vikuu binafsi na hasa vinavyomilikiwa na taasisi za kidini viliongezeka kwa kasi, huku taasisi zote zinazotoa elimu ya juu nchini hata kama siyo vyuo vikuu kuingizwa katika orodha ya kunufaika.

# Kundi wanaofeli kidato cha pili Katavi wanakimbia kurudia wakikwepa aibu

INATOKA UK.11

28, watano wamehamia shule nyingine.

"Baadhi wamechelewa kuripoti shuleni kwa sababu ya kuona aibu, pamoja na sababu zingine lakini sababu kubwa ni kuona aibu. Kimsingi, mimi nafundisha darasani, wanafunzi hao waliorudia wameonekana sasa kujitambua na wanafanya vizuri.

"Hawa wanafunzi 26 bado hawajarudi mpaka sasa tunaendelea kufuatilia sababu tuko mwishoni sana kwenye usajili, ili tujue sababu ya kutokurudi shuleni kurudia, ni nini sababu lakini kwa sababu za haraka haraka, wengi wanaona aibu kurudia kukutana na wenzao waliokuwa kidato cha kwanza.

"Jitihada mojawapo tunazofanya ni kupeleka majina kwa (Ofisa) Mtendaji wa Kata, kama tunavyofanya kwa ambao hawajaripoti kidato cha kwanza. Maana hawa nao tunawahesabu kama hawajaripoti tunafanya hivyo, ili kutimiza lengo la serikali kuwa wanaoanza kidato cha kwanza, wamalize kidato cha nne kama walivyoanza.

Ndani yake kuna swali ujauzito je? Mkuu wa Shule anakiri kwa majibu: "Kweli tunayo taarifa ya mwanafunzi mmoja ambae inasemekana kua ana ujauzito, lakini kwa Manispaa ya Mpanda tuna kituo kinachoshughulika na wanafunzi wenye changamoto hiyo na tayari tulishawasiliana na Mratibu Elimu Kata, ambaye anasimamia kituo hicho cha Kashato."

"Tayari huyo mwanafunzi ameenda pale ameripoti na anaendelea na masomo, lakini taarifa za huyo mwanafunzi mzazi alikuja na tukamwambia aende Polisi," anasema, akimtaka mzazi amesharipoti na iandaiwa mhusika wa kiume ametoroka.



Wanafunzi wa Kituo maalum cha walioacha masomo kwa sababu tofauti, mjini Mpanda. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

### WAATHIRIKA

Mary (jina la pili tunalo), ni miongoni mwa wanafunzi waliokwama kwenye mtihani kidato cha pili na amekubali kurudia kuendelea na masomo, kama kawaida.

"Nilikuwa naomba na hao wengine ambao wapo nyumbani waliofeli kidato cha pili warudi shule kurudia, kwa sababu masomo tunaendelea kama kawaida, hakuna chochote kilichobadilika wala hatuchekani," anasema mwanafunzi Mary.

Mwingine kwa jina la Emelda, naye anaifafanulia Nipashe uamuzi wake, kwamba: "Niliamua mimi mwenyewe kurudia, kwa sababu niliwaza maisha ya mtaani sio mazuri.

"Unaweza kukaa mtaani ukapata mimba za utotoni, magonjwa kwa hiyo mimi nawashauri wenzangu walioko nyumbani warudi shule maisha ya mataani sio mazuri 'kivile'! Utayafurahia mwanzoni, lakini utakaposhiindwa, utajuta na kusema 'ningejua ningerudi shule.'

"Matokeo yalipotoka kiukweli niliumia kulia pia nililia, ila nilijipa moyo nikasema nirudi shule na nilikuja shule tarehe ya kufungua hiyo tarehe 9, tofauti na wenzangu... sikuteteleka na nikajipa moyo kuna mungu atanisaidia na ndoto yangu kubwa nahitaji kuwa Polisi," anasema Emelda.

Mwingine kwa jina Cecilia anasema: "Tulifanya mtihani, matokeo yalivyotoka kweli yametoka vibaya tumefeli na wengine waliomtaani nawahamasisha warudi shule ili waendelee na masomo watimize malengo yao," anadems, akiungwa mkono na mwingine, ambaye hakutaka kutajwa jina:

"Watu wanaogopa kuchekwa wanaogopa aibu. Mimi niwambie, hakuna mtu anaowacheka, sisi tumepokelewa vizuri na wenzetu na wametutia moyo wamesema tusome kwa bidii tuongeze juhudi tutafaulu hadi walimu wametutia moyo."

### ALIYEGOMA AFUNGUKA

Kaisi (jina lake tunalo), ni miongoni mwa wanafunzi waliofeli kidato cha pili, pia amegoma kurudi shule akitoa sababu kwamba, anahisi akifika shuleni atachekwa, kusemwa na kunyooshewa vidole, pia ataumia kuona aliosoma nao wako mbele yake kimasomo.

"Mimi naishauri serikali, mwanafunzi aliefeli sio lazima arudie wanaweza kuongeza kampuni vyuo vya ufundi anaefeli anaenda kujifunza mambo mengine kama mimi natamani niende kujifunza hata ushonaji wa nguo tu."

"Wanafunzi wengi hawarudii kuogopa kuchekwa, yaani hiyo ni kawaida, lazima tu utachekwa utasemwa ukipita watasema huyo hivi na unaweza kurudia halafu tena ukafeli, ndio maana nikawaza bora niende kujishughulisha na vitu vingine.

"Mimi sio kwamba nilifeli makusudi, mimi nilikuwa naweza kabisa, najua lazima nifaulu. Sasa ndio hivyo nashangaa imekuja kutokea nimefeli," anasema mwanafunzi huyo.

### NENO LA WAZAZI

Matrida Nicholaus, ni mzazi wa mtoto wao aliyegoma kurudi shule kurudia masomo kidato cha pili, akilalamika ametumia muda mrefu kumshawishi sana kumbembeleza mtoto wake kurudi shuleni pasipo mafanikio.

"Kasema yeye hawezi kurudia, anachotaka tumpeleke kwenye ufundi wa cherehani, labda (Nipashe) umuulize na yeye akikubali kurudia sisi wazazi wake tuko tayari kumsomesha.

"Alipogoma kwa walimu hatukwenda wala ngazi yoyote. Hatukwenda, kwa sababu mtoto mwenyewe tunamjua, akigoma amegoma, sababu anayesoma ni mtoto, unaweza kumlazimisha akawa hafiki shule tunafanyaje?

"Mtoto ndio muamuzi. Yeye ndio anayesoma, yeye ndie anayeacha shule, kwa hiyo akigoma huwezi kumlazimish. Aligoma baada ya kufeli. Natamani arudie shule, amalize lakini nafanya nini sasa, tumemwambia abadilishe shule, lakini haelewi. Mimi na baba yake tulimtenga baada ya kuona amefeli," anasema Matrida.

## WANENAVYO MALENGA

### KIUNO

Hizi kazi za kiuno, bora kuziangazia,
Zingine ni ngumu mno, kifanywa kwa kuzidia,
Hata kuleta mguno, na tena kali hisia,
Mwautaja moyo, kiuno ndicho chenyewe.

Ukitembea kiuno, miguu chashikilia,
Ukigeuka kiuno, nacho watumia,
Ukiinama kiuno, kikigoma unalia,
Mwautaja sana moyo, kiuno ndicho chenyewe.

Kitaka tamba kiuno, ndiyo unakitumia,
Unaiweka mikono, mikogo kufanyizia,
Kina dharau kiuno, makubwa chatufanyia,
Mwautaja sana moyo, kiuno ndicho chenyewe.

Ukiinuka kiuno, ndicho chakusaidia,
Kiungo bora kiuno, vile tunakitumia,
Hapa ninatia neno, kazi kukipunguzia,
Mwautaja sana moyo, kiuno ndicho chenyewe.

Kichezacheza kiuno, viungo wainulia,
Kizungukavyo kiuno, watu wanafurahia,
Kazi kubwa ya kiuno, wengine kuridhishia,
Mwautaja sana moyo, kiuno ndicho chenyewe.

Chakarika we kiuno, hivyo wanakutumia,
Kweli unachoka mno, kazi nani tamwachia?
U peke yako kiuno, kazi kwako yasalia,
Mwautaja sana moyo, kiuno ndicho chenyewe.

Ungekuwa ni mkono, uko mwingine kulia,
Huu ukiwa na neno, kwingine badilishia,
Ni wa pekee kiuno, wala usijetitia,
Mwautaja sana moyo, kiuno ndicho chenyewe.

Hata uzazi kiuno, kwako tunaangalia.
Kikifunguka kiuno, watoto wanatujia,
Kikijifunga kiuno, tunabaki tunalia,
Mwautaja sana moyo, kiuno ndicho chenyewe.

Mtu kiumwa kiuno, utamsikitikia,
Hana kazi ni maneno, akiwa anagumia,
Mengi yanakwama mno, alipo anabakia,
Mwautaja sana moyo, kiuno ndicho chenyewe.

Heshima pata kiuno, yote unatufanyia,
Kwa sababu ya kiuno, mizigo twainulia,
Usiugue kiuno, tuzidi kukutumia,
Mwautaja sana moyo, kiuno ndicho chenyewe.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Serikali yaombwa kuzifuta taasisi zinazohamasisha ushoga

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KANISA la Moravian Tanzania Parishi ya Sabasaba mkoani Singida limeiomba serikali kuzifuta taasisi zote zisizo za kiserikali ambazo zinatuhumiwa kuhusika kuhamasisha mapenzi ya jinsia moja.

Mchungaji wa kanisa hilo, Yona Ezekiel alisema hayo juzi wakati akihubiri katika Ibada ya Sikukuu ya Pasaka, huku akiangua kilio kanisani kwa kukelwa na vitendo vya ushoga na kueleza kuwa serikali ichukue hatua za haraka kuyafuta mashirika hayo.

Alisema hivi karibuni aliyekuwa Mbunge wa Kyela, Dk. Harison Mwakyembe alisema zipo taasisi nyingi ambazo zimeenea hadi mikoani ambazo zinahamasisha ushoga na wakurugenzi wa taasisi hizo wanajulikana na kuwa walengwa ni vijana.

"Tumeambiwa na Dk. Mwakyembe kuwa taasisi hizi zipo na wahusika nazo wapo tunaiomba serikali izifute kwani zina waharibu vijana ambao ni nguvu kazi ya taifa na Watanzania awahutaki ushoga, usagaji na ukatili wa kijinsia wa aina yoyote kwani na hata vitabu vya dini vimekataza mambo hayo," alisema.

Akihubiri huku akilia na kusababisha waumini wote kuangua vilio, Mchungaji Ezekiel alisema Tanzania isikubali kuingia katika vitendo hivyo kwa shinikizo la kupata fedha za mikopo kutoka kwa matajiri ambapo aliwaomba wazazi kuendelea kufuatilia nyendo za watoto wao ambao ndiyo wa engwa wa mambo hayo.

Mchungaji Ezekiel alitumia ibada hiyo kuwahimiza wakristo kuacha kutenda dhambi na badala yake kuwa na moyo wa huruma wa kusaidia watu mbalimbali wenye uhitaji.

Aidha, aliwahimiza wakristo wa kanisa hilo kujitokeza kwa wingi kwenye Mkutano wa Umoja wa Makanisa mkoani hapa ambao utaanza kwa maandamano yatakayoanzia katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Usharika wa Mitunduruni kupitia Barabara ya Kinyeto, TRA, Barabara ya Arusha hadi eneo utakapofanyika mkutano huo.

Alisema Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Katika hatua nyingine Mchungaji Ezekiel aliwaomba wadau mbalimbali kusaidia ununuzi wa kiwanja cha kujenga Kanisa la Moravian Parish ya Sabasaba kwani hivi sasa wanafanya ibada zao katika kanisa la muda walilolijenga kwa kutumia miti na mabati.

# EWURA yawaonya waagizaji, wauzaji wa vilainishi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetoa onyo kwa waagizaji, wasambazaji na wauzaji wa vilainishi visivyokidhi ubora kwamba watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo faini na vifungo.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile alitoa onyo hilo jijini hapa mwishoni mwa wiki baada ya hivi karibuni kuwapo na uuzaji wa vilainishi hivyo kwa baadhi ya maeneo nchini kinyume na sheria.

Alisema kwa mujibu wa Kanuni ya 56(1) ya Kanuni za Petroli (shughuli za vilainishi), mwaka 2022 mfanyabiashara atakayekutwa na vilainishi visivyokidhi ubora atachukuliwa hatua za kisheria kwa kutozwa faini ya Sh.milioni 10 kwa atakayezalisha vilainishi.

"Atakayebainika kuuza vilainishi visivyokidhi ubora faini ni Sh.milioni saba na msambazaji faini ni sh.milioni sita na Sh.milioni tano kwa muuzaji wa rejareja, hizi adhabu zinaambatana na vifungo mbalimbali kwa mujibu wa sheria,"alisema.

Alisisitiza: "Hivyo basi, EWURA inatoa onyo kwa wazalishaji, waagizaji, wauzaji wa jumla na wasambazaji wa vilainishi kuacha mara moja kuuza bidhaa zisizokidhi ubora kwa kuwa ni kinyume cha sheria."

Aidha, aliwataka wauzaji wa vilainishi kuhakikisha wamesajili vilainishi vyao kwa EWURA kabla ya Mei 15, mwaka huu.

Alisema: "EWURA inatoa wito kwa wananchi kudai stakabadhi ya malipo kila wanaponunua vilainishi na kuwasiliana na EWURA kwa simu ya bure 0800110030 pale watakapobaini uwepo wa vilainishi visivyokidhi viwango".



Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Kasilda Mgeni (wa pili kulia), akijadiliana jambo na Ofisa Utalii wa Hifadhi wa Taifa ya Mkomazi, Happiness Kiemi alipotembelea hifadhi hiyo kuhamasisha utalii wa ndani, mwishoni mwa wiki. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Viongozi wa dini wataja chanzo mmomonyoko wa maadili

**Ibrahim Joseph na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa dini mkoani Dodoma wamesema kuwapo kwa mmonyoko wa maadili kwa jamii unachangiwa na ukosefu wa malezi, kwamba taifa lina kazi kubwa ya kurejesha maadili kwa jamii hasa kwa vijana.

Hivyo, wameiomba serikali kuyafutia usajili mashirika na taasisi zitakazoonekana kuhamasisha vitendo vya ndoa za jinsia moja.

Wakizungumza juzi kwa nyakati tofauti katika Ibada ya Pasaka, walisema ni wakati wa jamii kuchukua hatua ya kurejesha maadili na siyo kuiachia pekee serikali kwa kuwa jukumu la malezi lipo kwa wazazi na walezi.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kirutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Askofu Amon Kinyunyu, alisema mitandao ya kijamii, makundi yasiyokuwa na maadili yamekuwa wakifundisha vijana kuvuta bangi na kushiriki matendo mabaya kwenye jamii.

Alisema ni muhimu wazazi kujenga taifa lenye maadili na kuacha kuiga tamaduni za nje.

Kadhalika alisema baadhi ya mashirika na taasisi zinazojificha kwenye mwamvuli wa neno la Mungu zinatumika kuharibu maadili ya vijana kwa kitu kinachoitwa haki.

Naye, Askofu Mkuu wa Kanisa la Karimali Assembles of God Tanzania, Dk. Evance Chande ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maaridhiano Mkoa wa Dodoma, alisema kuwa wazazi na walezi wamekuwa chanzo kikubwa cha mmomonyoko wa maadili kutokana na baadhi yao kuwafundisha tamaduni za kutoka mataifa ya nje.

"Unaweza kukuta mzazi au mlezi anatoka nyumbani na mtoto wake huku mzazi, mlezi akiwa amevaa nguo zinazoonyesha viungo vya ndani bila kujali kuwa mtoto huyo anaweza kujifunza tabia hiyo ambayo inayoweza kumletea madhara badae," alisema.

Aliwahimiza Watanzania kutunza mazingira na kufanya usafi na kwa kufanya hivyo ni sehemu ya ibada kwani hata Mungu anasisitiza juu ya utunzaji wa mazingira.

Katika hatua nyingine, Kasisi wa Kanisa la Anglikana Parish ya Mlimwa C Dodoma, Julias Kiswagala, aliomba serikali kuchunguza kwa misaada inayoletwa na mashirika na taasisi kwa Watanzania ili kudhibiti yanayotoa kwa ajili ya kuchochea ndoa za jinsia moja.

Alisema: "Hata kama wao wanaleta fedha na misaada mbalimbali kwa ajili ya Watanzania bado serikali inatakiwa kuangalia kwa jicho la pili kwa kuwa wasipofanya hivyo watoto na vijana wanaweza kuharibikiwa ambao ni nguvu kazi ya taifa".





# Viongozi wa siasa, dini, serikali wadaiwa kuharibu mazingira

**Na Nebart Msokwa,**
CHUNYA

WAKAZI wa Kata za Sangambi na Chalangwa wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, wamewatuhumu viongozi wa dini, vyama vya siasa na serikali kuwa ndiyo vinara wa kuharibu mazingira katika maeneo yao kwa kufanya shughuli za kibinadamu kwenye misitu.

Wamesema viongozi hao wamekuwa wakiuza misitu iliyohifadhiwa, kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa na baadhi yao wanaendesha shughuli za kilimo kwenye misitu hiyo hali ambayo inahatarisha uwepo wa misitu hiyo.

Walitoa tuhuma hizo mwishoni mwa wiki kwenye mkutano wa hadhara wa pamoja kati ya Kijiji cha Idendeluka kilichopo Kata ya Sangambi na Mponela kilichopo Kata ya Chalangwa.

Mkutano huo pia uliwahusisha viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, maofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini na mila pamoja kutoka pande zote mbili.

Mmoja wa wananchi hao, Christopher Kalinga ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Idendeluka alisema viongozi wa serikali ya kijiji chao ndio vinara wa kuharibu mazingira jambo ambalo walitakiwa wawe mstari wa mbele kuzuia.

Alisema wamekuwa wakifyeka misitu na kulima pamoja na kuchoma mkaa kwa ajili ya kuuza kwa vijana wa bodaboda wanaotoka Mbeya Mjini.

"Tunapowachagua hawa viongozi huwa tunategemea kwamba wao ndio watatuongoza katika kutunza mazingira, lakini sasa wao ndio wanaongoza kufyeka misitu, wanachoma mkaa na hata hapa kwenye mkutano wapo," alisema Kalinga. Naye Mpoka Kilinga, alisema ili kupunguza uharibifu wa mazingira katika maeneo hayo, serikali inatakiwa kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kilimo, makazi ya binadamu na maeneo ya misitu iliyohifadhiwa.

Pia aliiomba serikali kuweka sheria ngumu ambazo zitasaidia kuwadhibiti waharibifu wa mazingira hasa wanaochoma mkaa kwenye vijiji vyao, akisisitiza kuwa madhara ya uharibifu huo yatakuwa makubwa.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sangambi, Ntundu Chapa alisema yapo baadhi ya maeneo ambayo yalitengwa kwa ajili ya misitu ya hifadhi lakini wahuni wamevamia na wanafanya shughuli za kibinadamu hasa uchomaji wa mkaa.

Ofisa Misitu kutoka TFS Wilaya ya Chunya, Innocent Lupembe alisema walitembelea maeneo mbalimbali ya kata hizo na kubaini uharibifu mkubwa wa misitu ukiwa unaendelea kufanywa na wananchi.

Alisema katika baadhi ya maeneo walibaini wananchi wakiendesha kilimo kwenye misitu na wengine wakikata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde aliagiza Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwasweka ndani viongozi wote waliotajwa na wananchi wa maeneo hayo kuwa washiriki kuharibu mazingira.

Alisema athari za uharibifu wa mazingira zimekuwa zikiongezeka kila mwaka na kuleta madhara duniani na hivyo akawataka wananchi kujiepusha na uharibifu wa mazingira.

Aliwataka wananchi wa maeneo hayo kuendelea kulinda misitu huku akiwataka maofisa wa TFS kuwapatia motisha wananchi wanaohifadhi vizuri mazingira.




Kijana mwenye ualbino akitoa ushuhuda mbele ya waumini wa kanisa Katoliki la Bikira Maria wa Fatima Parokia ya Mwanjelwa Jimbo Kuu la Katoliki Mbeya juzi, kuhusu namna alivyonyanyapaliwa na ndugu zake akiwa mdogo huku akiwa amebeba bango la kuwaomba msaada kuchangia ili kukabiliana na tatizo la saratani ya ngozi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali yawatangazia kiama walanguzi maparachichi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI wilayani Rungwe mkoani Mbeya, imetangaza kiama kwa wafanyabiashara walanguzi wa maparachichi kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Amesema bei elekezi ya zao hilo kwa msimu huu ni Sh. 1,600 kwa kilo moja.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu alitoa tahadhari hiyo kwenye mkutano maalumu na wakulima wa maparachichi pamoja na wadau wa kilimo cha zao hilo wakiwemo mawakala na kampuni ya ununuzi wa zao hilo.

Alisema kuanzia msimu huu wanunuzi wote wa maparachichi lazima wanunuwe zao hilo kwa kufuata utaratibu uliowekwa na kwamba watakaokiuka watachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kupelekwa mahakamani.

Alisema wanunuzi wote wa maparachichi wanatakiwa kuwa na vitambulisho vya kampuni wanayotokea ili kuepuka wahuni kutumia mwanya huo kuendelea kuhujumu biashara ya zao hilo.

Alisema ununuzi holela wa zao hilo umekuwa ukichochea baadhi ya watu kuiba matunda ya watu wengine na kuyauza jambo ambalo limekuwa likisababisha migogoro isiyokuwa ya lazima.

"Lakini pia kuna tabia ya wanunuzi kuchuma maparachichi ya wakulima na kuanza kuyachambua kwa kuchukua mazuri na mengine wanayaacha wakidai ni 'reject' hii tabia siihitaji kabisa maana inawaharibia wakulima," alisema Haniu.

Alisema mtu yeyote atakayekamatwa ananunua maparachichi kwa kukiuka maelekezo aliyoyatoa atakamatwa na polisi na kufikishwa mahakamani.

Alisema kampuni ambayo hayatakuwa tayari kufuata utaratibu ni bora zijiondoe kwenye biashara hiyo ili wakulima watafutiwe kampuni zingine za uhakika ambayo alisisitiza kwamba yapo na yako tayari kufanya biashara katika wilaya hiyo. Baadhi ya wakulima walisema wamekuwa wakidhurumiwa na wanunuzi wa zao hilo kutokana na kutokuwepo kwa utaratibu mzuri wa ununuzi wakidai kuwa baadhi ya madarali wamekuwa wakichuma matunda na kuondoka nayo bila kuwalipa.

Mmoja wa wakulima hao, Boneka Mwakyusa alisema hivi karibuni kuna watu walichuma matunda yake na kuchambua mazuri kisha yaliyobaki wakawa wananunua mfuko mzima kwa Sh. 600 jambo ambalo alidai linawaumiza.

Alisema maparachichi yakishachumwa thamani yake huwa inashuka endapo hayatanunuliwa na wateja tofauti na mazao mengine zikiwemo ndizi.

Alisema hata bei ambazo huwa wanauza matunda hayo huwa zinatofautiana kulingana na kampuni ambapo alisema hakuna kampuni inayonunua kwa bei kama aliyoitaja Mkuu wa Wilaya.

"Wamekuwa wakinunua kwa kati ya Sh. 1,000 na 1,300, tunashukuru kwa maelekezo ya Mkuu wa Wilaya na tunaamini hii itatusaidia kuinua kipato chetu, wamekuwa wakituumiza.

Hata hivyo baadhi ya wanunuzi walisema wamekuwa wakichambua matunda baada ya kuchuma kutokana na wakulima wengi kutofuata njia bora za uzalishaji na hivyo kusababisha baadhi ya matunda kuwa mabovu.

Walisema wakulima wanachanganya maparachichi na migomba kwenye shamba moja jambo ambalo linasababisha matunda yao kukosa ubora.

## Jamii yashauriwa kutowatenga waraibu dawa za kulevya

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

JAMII imetakiwa kutowatenga waraibu wa dawa za kulenya na badala yake iwatie moyo na kuwaelimisha ili waliotayari kuacha matumizi ya dawa hizo waache na washiriki kwenye ujenzi wa taifa.

Mtaalamu wa Saikolojia wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya Kliniki ya waraibu wa dawa za kulenya, Betuna Mwamboneke aliyasema hayo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu matibabu ya waraibu hao.

Alisema jamii inatakiwa kuendelea kuwatia moyo na kuwahimiza waraibu wa dawa hizo ambao wanaendelea na matibabu kwenye vituo mbalimbali ili wasiondoke kwenye tiba hizo

Mwamboneke alisema jamii imekuwa ikiwanyanyapaa waraibu wa dawa za kulenya, hivyo kuwafanya waendelee kuwa kutumia dawa hizo na hata wanaohitaji msaada wa matibabu ya kuachana na dawa hizo wanakosa kuungwa mkono.

Alisema hali hiyo inatokana na waraibu wengi kujihusisha na vitendo vya uhalifu ikiwemo wizi na ubakaji hali iliyosababisha jamii kudhani kundi hilo halina faida yoyote.

Alisema malezi yana mchango mkubwa kwa jamii, hivyo wazazi na walezi wanapaswa kuanza kutoa elimu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya kwa watoto wao kwa maelezo kuwa baadhi ya wathirika wameanza matumizi ya dawa hizo wakiwa katika umri mdogo.

Alieleza sababu za vijana wengi kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulenya kuwa ni pamoja na ugumu wa maisha, kutaka kupunguza maumivu, migogoro ya ndoa na familia, malezi yasiyo bora, matatizo ya kimwili pamoja na upatikanaji wa dawa hizo.

Aliongeza kuwa elimu inapaswa kutolewa kwa vyombo vya usalama kujua umuhimu wa matibabu ya kisaikolojia kwa waathirika hao ili kuwasaidia kupata matibabu hata wanapokuwa wanatumikia adhabu mbalimbali.

Alishauri serikali kuongeza mikakati ya kuwatengenezea matibabu waraibu ikiwa ni pamoja na kuongeza vituo vya ushauri tiba kwa maelezo kuwa wanaofikiwa na huduma hizo ni wachache ukilinganisha na idadi ya waraibu waliopo.





## Benki ya Exim yatoa msaada wa chakula kwa maskini

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BENKI ya Exim Tanzania imetoa msaada wa chakula na mahitaji muhimu kwa kaya maskini 19 visiwani Zanzibar pamoja na kuandaa futari kwa wateja wake visiwani humo.

Tukio hilo ni mwendelezo wa benki hiyo kuwa karibu zaidi na wateja wake wenye imani ya Kiislam katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Matukio hayo yalifanyika mwishoni mwa wiki visiwani humo ikishuhudiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Hamza Hassan Juma aliyeongoza utoaji wa msaada kupitia Jumuiya ya Shauri Moyo Development Foundation.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Idara Maalum za SMZ, Massoud Ali Mohammed akiongoza hafla ya futari.

Mkuu wa Idara wa Masoko na Mawasiliano Benki ya Exim, Stanley Kafu alisema yanalenga kuiweka karibu zaidi benki hiyo na wateja wake.

"Tumekuwa tukiheshimu sana Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kutokana na ukweli kwamba, ni kipindi ambacho mwanadamu anajiweka karibu na Mungu wake kupitia mfungo na kufanya maombi."alisema.

Stanley aliahidi ushirikiano zaidi baina ya benki hiyo na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuhakikisha uhusiano uliopo baina ya benki hiyo na wafanyabiashara pamoja na wadau wa sekta ya utalii visiwani humo unaendelea kuboreshwa.

Wakizungumza kwenye matukio hayo Waziri Hamza Hassan na Waziri Masoud Ali Mohammed kwa nyakati tofauti waliipongeza benki hiyo kwa kuandaa matukio hayo wakiahidi kuendeleza ushirikiano na benki hiyo.

Alisema: "Kwa matukio mliyoyafanya hii leo visiwani Zanzibar mnadhihirisha dhamira yenu njema ambayo siyo tu kuhudumia jamii hii ya Wazanzibar kupitia huduma zenu za kibenki bali pia kushirikiana nao hata kwenye masuala yanayohusu imani yao".

# Barabara Chakechake-Wete yaanza kujengwa kwa vipande

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

UJENZI wa Barabara ya Chakechake-Wete kisiwani Pemba imeanza kujengwa vipande vipande kutokana na baadhi ya wamiliki wa nyumba zilizopaswa kubomolewa ili kupisha ujenzi huo kudai kutolipwa fidia.

Malipo ya fidia ya nyumba zinazotakiwa kuvunjwa yalianza kufanyika Febuari mwaka huu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mhandisi wa mradi huo toka kampuni ya ujenzi ya Mecco, Nassor Ramadhan, alisema wamelazimika kuendelea na ujenzi wa barabara hiyo vipande vipande ili kuokoa muda wa kukamilisha ujenzi huo.

"Tunalazimika kujenga vipande vipande kwa sababu kuna baadhi ya wananchi wanalalamika nyumba zao hazimo katika orodha ya malipo. Hatuwezi kuvunja nyumba zao kabla malipo kufanyika" alisema Mhandisi Nassor.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo unatakiwa uwe umekamilika ndani ya miezi 30 kwa mujibu wa mkataba.

Barabara hiyo ina upana mita tisa na urefu wa kilomita 22 inaanzia Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba hadi wilayani Wete Mkoa wa Kaskazini kisiwani humo.

Hata hivyo alisema kuna tatizo lingine limejitokeza na kusababisha kazi kuwa kubwa na kuongezeka kwa asilimia 300 baada ya kulazimika kupasua milima na kuondosha udongo usiohitajika kutokana na mazingira ya jiografia ya milima, mabonde na udongo kuwa wa ufinyazi katika sehemu inayopita barabara hiyo.

"Tunalazimika kuondosha udongo wa ufinyanzi na kushindilia udongo mwingine toka nje ya eneo la mradi kwa sababu udongo wa mfinyanzi haufai katika ujenzi wa barabara. Endapo mdongo mfinyanzi ukitumika utasisababisha barabra kupasuka," alisema.

Alisema kiwango cha barabara kinahitaji ubora wa udongo, ndiyo maana wanashindilia kifusi cha mawe na baadae kumwagwe kokoto kabla ya kuwekwa lami.

Hata hivyo alisema wapo baadhi ya wananchi wamelipwa fidia lakini nyumba zao bado hawajaanza kubomoa na walipoulizwa walisema kukawia kwao kumetokana na mfungo wa Mwezi wa Ramadhani.

Mhandisi Nassor alisema ujenzi wa barabara hiyo unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (BADEA) ambapo Sh. bilioni 23 zinatarajiwa kutumika katika ujenzi huo.

Kwa upande wa wananchi wanaolalamika bado hawajalipwa fidia katika Kijiji cha Mzambarau Takau, kwa nyakati tofauti walisema nyumba zao zilihakikiwa mara mbili lakini katika ulipaji wa fidia majina yao hayamo jambo ambalo limewashtua.

"Nyumba yangu ilifanyiwa uhakiki mara mbili lakini cha ajabu katika orodha ya malipo ya fidia nyumba yangu haimo .Jambo hili limenishtua na kunipa mshangao, "alisema Shavua Ali.

Naye Nassor Ali Hamad mkazi wa kijiji hicho, alisema kuna nyumba 682 ambazo zipo katika mtaa mmoja zimenufaika na malipo ya fidia wakati nyumba namba 651 na 652 hazimo katika orodha ya malipo.

Mwenyekiti wa Msikiti wa Patini, Kombo Shavua alisema msikiti wao umeingizwa katika orodha ya kuvunjwa lakini katika orodha ya mwisho ya malipo msikiti huo haumo.

"Mskiti wetu namba 654 umo katika ramani ya nyumba zinanazotakiwa kuvunjwa lakini katika orodha ya malipo msikiti huo haukujumuishwa. Tunaiomba serikali iliangalie kwa kina suala hili,"alisema.

Sheha wa Mzambarautakao, Bakari Seif Juma alisema ni kweli kuna malalamiko ya wananchi ambao bado hawajalipwa fidia licha nyumba zao kuhakikiwa mara mbili.

Alisema Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Mawasiliano, Ujenzi, Uchukuzi na Usafirishaji Pemba, Ubrahim Saleh Juma baada ya kupokea malalamiko alifanya ziara maalum ya kukutana na wananchii ambao hawajalipwa fidia na kuwataka wawe na subira wakati suala lao linaendelea kufuatiliwa.



Mhandisi wa kampuni ya ujenzi ya MECCO, Nassor Ramadhan akizungumza na waandishi wa habari, ofisini kwake Mzambarau Takau Pemba jana, kuhusu maendeleo ya ujenzi wa Barabara ya Chakechake hadi Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Ofisi ya Mufti yatakiwa kutoa mafunzo ya ndoa kulinda mila

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Mufti Mkuu wa Zanzibar imetakiwa kuendelea kutoa mafunzo ya ndoa yanayolinda mila, silka na utamaduni ili kuifanya Zanzibar ibaki katika misingi ya maadili.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed alitoa wito huo wakati akiyafunga mafunzo ya ndoa ya awamu ya 17 yaliyofanyika katika Masjid Jamiya Zenjibar Mazizini Zanzibar.

Alisema ofisi ya Mufti ina kazi kubwa katika kuwajenga walengwa kuwa na maadili mema na kuhakikisha ndoa zinadumu kwa muda mrefu kwa kutoa mafunzo yanayoendana na silka na tamaduni.

Aidha, alisema miongoni mwa sababu zinazosababisha kuvunjika kwa ndoa nyingi ni pamoja na kutokuwepo kwa uwaminifu baina ya wanandoa, kukosekana kwa uvumilivu ndani ya ndoa.

Alitaja sababu nyingine ni kukokesekana kwa upendo wa dhati, kukiuka mafundisho na miongozo ya dini pamoja na watu kukosa hofu na imani ya dini katika suala la ndoa.

Alisema utafiti unaonesha kuwa ndoa nyingi zinazovunjika ni zile ambazo baina ya mwaka wa kwanza hadi mwaka wa tano kunakosababishwa na vijana kwa kukosa taaluma sahihi ya ndoa.

Alisema katika kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazozikabili ndoa kuna haja kwa ofisi ya Mufti kuelezea kwa upana wake madhara ya talaka katika jamii na husababisha kukosekana kwa watoto wenye maadili mema sambamba na kukosekana kwa huduma muhimu kwa watoto ikiwemo malezi bora.

Katibu Mtendaji ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar, Khalid Ali Mfaume alisema ofisi hiyo inasimamia mafunzo kwa walimu wa madrasa na kutoa leseni kwa walimu waliofaulu katika kutoa mafunzo ya ndoa.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu wenzake, Ukhuti Asya Wadi Makame alisema wanaishukuru ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibr kwa kuratibu mafunzo hayo.

# Viongozi dini walaani mmomonyoko maadili

**Na Ashton Balaigwa**, MOROGORO

VIONGOZI wa dini mkoani Morogoro, wamelaani mmomonyoko wa maadili kwenye jamii ikiwamo vitendo vya ushoga na ukatili wa kijinsia ambavyo havikubaliki na kutaka Watanzania kusimamia misingi imara ya maadili, mila na desturi ili kujenga taifa lenye kumcha Mungu.

Walitoa kauli hizo kwenye Ibada Sikukuu ya Pasaka iliyofanyika makanisa tofauti mkoani Morogoro.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Morogoro, Jacob Ole Mameo, aliwataka waamini kufanya toba ya kweli ili vitendo hivyo vitoweke kwa kuwa vinatishia na kuleta sura mbaya kwa nchi.

Askofu Mameo alisema waamini wafanye toba pia kwa ajili ya kuepusha nchi kupata majanga ikiwamo ukame, mafuriko na magonjwa ambayo hutokana na machukizo ya binadamu.

Askofu Godfrey Seheba wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Morogoro, aliwataka Watanzania bila kujali dini wala kabila kufanya maombi kwa ajili ya kuepusha nchi kuingia katika majanga mbalimbali ikiwamo magonjwa yanayotokea nchi za jirani.

Askofu mstaafu wa Jimbo Katoliki Morogoro, Telesphor Mkude, aliwataka Watanzania kusimamia misingi imara ya maadili mema, mila na desturi nzuri zilizopo ili kujenga taifa lenye kumcha Mungu.

Akitoa ujumbe wa Pasaka wakati akihubiri katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Patrice mjini Morogoro, alisema ni muhimu jamii kuacha kuchanganya mila na desturi ambazo hazifai katika taifa na zinazokwenda kunyume kwa kumcha Mwenyezi Mungu.

Alisema ni wajibu kwa waamini wa kanisa hilo na jamii kuendelea kuishi kwa kufuata maadili mema na kupinga vikali vitendo viovu vinavyotendeka ndani ya jamii.

Alivitaja baadhi ya matendo hayo maovu utoaji mimba, kuua watoto wachanga na watu wenye ualbino.

Alisema mengine ni kwa yale ambayo kwa kiasi kikubwa yamekuwa wakimchukiza Mungu hususani kwa mila ambazo haziendani na utamaduni wa Mtanzania.

Alisema Mungu aliwaumba kwa mfano wake na huo ndiyo upendo kama Muinjili Yohani anavyofafanua kwenye waraka wake wa kwanza kwa watu wote sura ya 4 mstari wa 16 "Mungu ni upendo".

Baadhi ya waumini wa kanisa hilo akiwamo Andrian John, alisema ni wajibu wa wazazi kuwalea watoto kwa kufuata misingi mizuri ya kimaadili ili waweza kujiepusha na kuiga utamaduni usiofaa kutoka katika nchi za kimagharibi.

Naye muumini Rose Mwilingo wa Kanisa la KKKT, alisema Watanzania wayatumie mafundisho wanayopata katika kipindi cha Pasaka kupigania kurejesha maadili ya kitanzania.




Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika akizungumza na wandishi wa wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2021/2022, akimtaka Rais Samia Suluhu Hassan kuchukua hatua ya kuwawajibisha waliofuja fedha za umma. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## STAMICO kusaidia wachimbaji wadogo

**Na Faustine Feliciane**

KAMPUNI ya GF Trucks & Equipment kwa kushirikiana na Shirika la Madini nchini (STAMICO), wameingia makubaliano kuwasaidia na kuwainua wachimbaji wadogo wa madini kwa kuwakopesha mitambo ya kuchimba.

Makubaliano hayo yamefanyika ili kuwapa uwezo wachimbaji wadogo kuinua kipato chao na kuongeza pato la taifa.

Akizungumza wakati wa kusaini makubaliano hayo, Mkurugenzi wa Masoko na Mawasiliano wa GF Truck, Salman Karmali, alisema wamegundua wachimbaji wengi wadogo hawana mitaji ya kununua mitambo hiyo na kuamua kuingia makubaliano na STAMICO kuwakopesha au kuwakodisha mitambo maalumu ya kuchimbia kwa gharama nafuu.

Alisema STAMICO kama walezi wa wachimbaji madini nchini ni rahisi kumtambua mhusika mwenye mahitaji na kwa kufanya hivyo kutapunguza ajali nyingi zinazotokea migodini kwa wachimbaji kutumia njia za asili badala ya njia za kisasa.

"GF Truck tumekuja kama mkombozi wao kupitia mitambo ya XCMG tutakua tumetatua changamoto zao kwa kiwango kikubwa, itasaidia sana kuwaongezea tija kwenye shughuli zao," alisema Karmali.

Aidha, alisema kwa kushirikiana na STAMICO wataweka utaratibu mzuri kwa wachimbaji hao wadogo kupata huduma hizo walizozianzisha.

Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Venance Mwasse, alisema mpango huo utawasaidia zaidi wachinbaji wadogo kufikia lengo kujiongezea kipato na kufanya shughuli za uchimbaji kisasa.

Akizungumza kwa niaba ya wachimbaji wadogo, Naumia Mwakasita, kutoka mgodi wa Chunya mkoani Mbeya, alisema huduma hiyo ni fursa kwao iliyokuja kuwakomboa na hali ya kutumia vifaa duni katika uchimbaji.

# CAG abaini wanafunzi 23,000 kukatisha masomo kwa mimba

**Na Godfrey Mushi**, DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2021/22, imebaini katika Mamlaka 19 za Serikali za Mitaa, wanafunzi 23,009 wamekatisha masomo yao shule za sekondari kutokana na ujauzito, huku Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ikiongoza.

Katika shule za msingi, wanafunzi 19,945 hawakumaliza masomo kutokana na sababu hiyo.

Ripoti hiyo, imebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, inaongoza kwa wanafunzi wake kukatisha masomo wakiwamo 9,045, ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, walioacha masomo 2,172.

Kwa mujibu wa Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa Serikali za Mitaa (LGAs) ya mwaka 2021/22, CAG Charles Kichere, alibaini wanafunzi wa sekondari waliokatisha masomo ni sawa na asilimia 28, kati ya 82,236 waliojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2018 na kutakiwa kuhitimu mwaka 2021.

Kwenye ripoti hiyo, CAG ameeleza sababu za kukatisha masomo zilikuwa ni pamoja na ujauzito kwa wanafunzi wa kike, umbali mrefu kutoka makazi ya wanafunzi hadi shuleni, malezi ya familia na sababu binafsi.

Ripoti hiyo inaonyesha kila halmashauri na idadi ya wanafunzi waliokatisha masomo kwenye mabano ni Kinondoni (4,652), Mji Newala (3,783), Misungwi (2,570), Morogoro (1,948) na Moshi (1,270).

Nyingine Kilosa (1,246), Temeke (1,185), Buhigwe (908), Gairo (700) na Mpanda (691).

Shule nyingine ni Tandahimba (685), Kalambo (669), Mwanga (536), Busokelo (468), Newala (453), Kigamboni (426), Mji Masasi (392), Makete (382) na Monduli (45).

Wakati kwa shule za msingi ni Gairo (1,365), Kwimba (9,045), Uvinza (2,172), Kilosa (2,096) na Nsimbo (1,545).

Alizitaja nyingine ni Kibondo (1,416), Kibaha (806), Morogoro (641), Mwanga (460), Newala (345), Makete (54).

Kutokana na tatizo hilo, CAG alipendekeza kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), iandae programu za kuzifikia jamii husika, kuhimiza wazazi na walezi kuwaandikisha wanafunzi katika shule zilizo karibu.

Aidha, alipendekeza serikali za mitaa kujenga shule mpya karibu na vijiji, kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, kwa kujumuisha vifaa vinavyofaa vya kufundishia na kujifunza, kuhimiza michezo na kutoa elimu ya taaluma na ufundi stadi.

## HABARI KIMATAIFA

# Zelensky, aahidi utulivu Pasaka ijayo

**KYIV,** Ukraine

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky ameshutumu mashambulizi ya anga ya Russia yalioangukia maandalizi ya Pasaka ya wa Orthodox juzi, ikiwa ni pamoja na lile lililowauwa baba na binti yake huko Zaporizhzhia, huku akiahidi wananchi wake kwamba Pasaka ijayo itakuwa na utulivu.

Katika utaratibu wake wa kulihutubia taifa kila jioni na siku muhimu kwa waukraine, Zelensky alibainisha kwamba usiku wa kuamkia jana, jeshi la Russia lilishambulia huko Zaporizhzhia kwa makombora ya S-300.

Alisema tukio hilo ni mfululizo wa makombora yaliyopiga katika makaazi na kuuwa watu watatu akiwemo mwanaume (50), mwanamke na mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 11, akishutumu kwamba hivyo ndivyo serikali ya Russia inavyoadhimisha sikukuu hiyo.

Pia Rais Zelensky, alivipongeza vikosi kadhaa vinavyolinda maeneo ya mashariki mwa nchi hiyo, huku akisema ana matumaini makubwa katika sherehe kama hizo, na kwamba mwaka ujao Ukraine itakuwa huru.

"Natumaini mwaka ujao itafanyika kwa uhuru na amani kwa watu wetu wote," alisema.

Katika taarifa ya Mkuu wa majeshi wa Ukraine, alisema kwamba zaidi ya mashambulizi 40 ya adui yamezuiliwa katika muda wa saa 24 zilizopita.

Aliongeza kuwa majeshi ya Russia yalianzisha mashambulizi ambayo hayakufanikiwa katika maeneo ya magharibi mwa Bakhmut ambayo imeharibiwa katika kiwango kikubwa.

"Russia pia haijafanikisha mashambulizi yake huko Avdiivka, eneo lingine la kimkakati ambalo linalengwa na vikosi vya Moscow katika uwanja wa mapambano huko Mashariki," alisema.

Hata hivyo, vikosi vya Ukraine vilisema vitaendelea kuilinda Bakhmut dhidi ya mashambulizi ya mara kwa mara ya Russia, ingawa wiki iliyopita rais Zelensky alikiri kwamba kuna hatari ya vikosi vyake kuzingirwa na kurudishwa nyuma.

Msemaji wa jeshi upande wa Mashariki mwa Ukraine Serhiy Cherevatyi, aliiambia televisheni ya taifa hilo kwamba vikosi vya Russia vinajaribu kuchukua himaya ya jiji lao kwa gharama yoyote.

"Mapambano bado ni makali na tunaendelea na udhibiti wa mji huo wa kimkakati, vikosi vyetu vinarudisha nyuma adui na kumesababishwa uharibifu mkubwa," alisema.

Katika hatua nyingine wizara ya Ulinzi ya Russia ilisema vikosi vyake vimeharibu ghala lililokuwa na tani 70,000 za mafuta karibu na Zaporizhzhia pamoja na maghala mengine ya kuhifadhi makombora, risasi na silaha huko Zaporizhzhia na Mikoa ya Donetsk.

Taarifa hizo hazikuthibitishwa na Kyiv na badala yake walisisitiza katika kuendelea kupigania mipaka yake kwa uhuru wa Ukraine na watu wake hadi kufikia maadhimisho ya sikukuu ya Pasaka ijayo.

Kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani Papa Francis, alitoa ujumbe wa Pasaka katika uwanja wa Kanisa la Mtakatifu Petro kwa kuhimiza uharaka wa kufuata njia za amani na undugu.

Kiongozi huyo wa Kanisa Katoliki aliwahutubia waumini zaidi ya 100,000 na kuwaeleza kwamba vita na mateso duniani vimegubika sherehe za Pasaka.

Vile vile, alitoa wito wa kuishinda migogoro na migawanyiko na badala yake kufungua mioyo ya wanadamu kwa wale wanaohitaji zaidi.

Pia Papa Francis, aliwakumbusha waumini juu ya vita vya Ukraine, huku akiisisitiza jumuiya ya kimataifa kufanya jitihada zote ili kukomesha vita hivyo pamoja na migogoro yote inayochafua dunia kwa umwagaji damu yakiemo mataifa ya Lebanon, Haiti pamoja na Sudan Kusini. **DW**



Papa Francis akihutubia wakati wa misa ya Pasaka, iliyofanyika Vatican, juzi. **PICHA:MTANDAO**

## Kenya yazindua setilaiti

**NAIROBI,** Kenya

TAIFA la Kenya limezindua setilaiti yake ya kwanza, ikiwa ni miongoni mwa tukio la kihistoria kwa nchi hiyo kupitia mpango wake wa masuala ya anga.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kituo cha anga cha Kenya, Satelite hiyo iliyopewa jina Taifa 1, ilirushwa jana kwa kutumia roketi ya SpaceX falcon 9, kutokea kwenye kituo chake cha Vandenberg Space mjini Carlifonia nchini Marekani.

Taarifa hiyo ilibainisha kwamba hatua hiyo ni muhimu katika maendeleo ya teknolojia kwa taifa hilo na kwamba itachangia pakubwa katika mpango wa nchi hiyo kujenga uchumi kupitia anga.

Wizara ya ulinzi ya Kenya pia ilisema kuwa, satelite hiyo imebuniwa na kutengenezwa na wahandisi kutoka katika taifa hilo na kwamba itatumika kukusanya takwimu kuhusu kilimo na usalama wa chakula ikiwa ni miongoni mwa mambo mengine. **DW**

## Macron, mgogoro China na Taiwan haupaswi kuchochewa

**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa Ufaransa Emmanuel Macron amesema kuwa Ulaya haina nia ya kuchochea mgogoro wa Taiwan na kwamba inapaswa kuendelea na mkakati huru mbali na Washington na Beijing.

Macron (pichani) alirejea hivi karibuni akitokea China baada ya ziara ya kiserikali ya siku tatu ambako alipokelewa kwa shangwe na Rais Xi Jinping.

Aidha, inaelezwa kuwa China mwishoni mwa wiki iliyopita ilianza mazoezi karibu na Taiwan kwa kukasirishwa na mkutano kati ya Rais wa Taiwan Tsai Ing-Wen na Spika wa Baraza la wawakilishi la Marekani Kevin McCarthy iliofanyika Jumatano.

Inatajwa kuwa China inaiona Taiwan inayojitawala kidemokrasia kama himaya yake na haijawahi kuachana na msimamo wa kutumia nguvu ili kukifanya kisiwa hicho kuwa chini ya udhibiti wake, huku serikali ya Taiwan ikipinga vikali madai ya China.

Rais Macron katika maoni aliyotoa kwenye gazeti la Ufaransa Les Echos na Politico wakati wa ziara yake nchini China, alisema Ulaya haipaswi kuongeza kasi ya mzozo lakini kuchukua muda ili kuwa na msimamo thabiti kama nguzo ya tatu kati ya China na Marekani. **VOA**


### KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**AKIDA MWINJUMA WARIA**
anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya **BAJAJ TVS KING** yenye usajili namba **MC 821 AUQ**,
CHASSIS NAMBA: **MD6M14PK1F4A40999.**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/KIJ/RB/114915/2023**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AKIDA MWINJUMA WARIA**
anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISH CANTER** yenye usajili namba **T 216 DDW,**
CHASSIS NAMBA: **FH21GC551333.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/KIJ/RB/114921/202**

### KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**HERI JOSEPH SANGA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba TAE 144980 iliyotolewa Dar es salaam PCO mwaka 2019 July.kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/75133/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya MOSHI**
**Kituo cha KAHE Mkoa KILIMANJARO**
**Usimamizi wa mirathi Na 08/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ADAM ABDU WA MOSHI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ABDULRAHMAN MOHAMED AFIF**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 mwezi 04 mwaka 2023 kabla huyomwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 10 mwezi 03 mwaka 2023




### NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED
### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**MAHAKAMA KUU – MISC COMMERCIAL NA. 19/2018**
MTI INVESTMENT LIMITED __________MDAI
DHIDI YA
CHOBO INVESTMENT COMPANY LIMITED __________MDAIWA

**MM/ILANGALA – SHAURI LA MADAI NA. 09/2020**
MICHAEL LADISLAUS _______________________MDAI
DHIDI YA
MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU MASKANI MAGESA____________________________MDAIWA

**MAHAKAMA KUU YA MASIJALA YA MWANZA- SHAURI LA MADAI NA. 69/2020**
**(Inayotokana na kesi Na. 30/2019)**
SIDNEY THOMAS KAZI ____________________MDAI
DHIDI YA
MARGARITHA THOMASI KAZI_________________MDAIWA

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA KUU, MAHAKAMA YA MWANZO ILANGALA NA MAHAKAMA KUU MASIJALA YA MWANZA, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI MAGARI NA NYUMBA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | GARI MITSUBISHI FUSO T 568 DJH | YADI YA NYADHI INVESTMENT | 25/04/2023 SAA 2 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | GARI MITSUBISHI FUSO NA. T 741 DJJ | YADI YA NYADHI INVESTMENT | 25/04/2023 SAA 2 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | TELA - VIBERITI T 199 AJQ FIAT | YADI YA NYADHI INVESTMENT | 25/04/2023 SAA 2 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4 | GARI SCANIA T 452 ARV | YADI YA NYADHI INVESTMENT | 25/04/2023 SAA 2 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 5 | GARI TOYOTA CARINA TI NA. T 540 BKV | YADI YA NYADHI INVESTMENT | 25/04/2023 SAA 2 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 6 | NYUMBA PLOT NA. 249, BLOCK "U" | MTAA WA MITIMIREFU WILAYA YA NYAMAGANA MKOA WA MWANZA | 03/05/2023 SAA 2 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. KWA MALI INAYOHAMISHIKA, MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI.
2. KWA MALI ISIYOHAMISHIKA, MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0768-588155**

# KIDUKU ULINGONI TENA 'MFALME KWENYE UFALME WAKE' MORO

**Na Saada Akida**

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Twaha Kiduku, anatarajia kupanda ulingoni Aprili 22, mwaka huu, katika pambano dhidi ya Iago Kiziria wa Georgia, lililopangwa kufanyika katika Ukumbi wa Tanzanite mjini Morogoro.

**Kiduku atapanda ulingoni kwenye pambano hilo lililoandaliwa na Kampuni ya Promosheni ya Ngumi za Kulipwa nchini, Peak Time Media, huku likipewa jina la Mfalme kwenye Ufalme wake ikiwa ni mara ya pili kufanyika baada ya mwaka jana Kiduku kumchapa Alex Kabangu wa DR Congo kwenye ukumbi huo wa Tanzanite.**

Katika pambano hilo la mwaka huu lilodhaminiwa na Global Tv Online, Gazeti la Championi, Azam Tv, Robby One Pharmacy, CRD Bank, Creative Bee, Smart Gin, Msaka Tonge, Joza Hotel, Bongo Boxing Safari na Sweet Afrika, kiingilio kimetangazwa kuwa Sh. 10,000 jukwaa la kawaida, Sh. 30,000 VIP B huku VIP A ikiwa ni Sh. 50,000.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa pambano hilo kutoka Peak Time Media, Bakari Khatibu, alisema wamerudisha tena pambano la Mfalme kwenye Ufalme wake katika mkoa huo kwa mara nyingine kutokana na rekodi kubwa ya Kiduku katika mchezo huo huku akimpongeza kutokana na kucheza na mabondia wagumu mara zote.

Alisema pambano hilo kwao ni mara ya pili kufanyika na kwamba sababu kubwa ya kufanyika tena mkoani humo ni kutokana na rekodi ya Kiduku ndani ya mkoa wa Morogoro.

"Ukiangalia mara zote, Kiduku amekuwa akisifika kwa kuletewa mabondia wagumu na sisi kama Peak Time Media, tumemletea bondia mgumu hivyo akae akijua hakutokuwa na 'kitonga' cha aina yoyote.

"Ni waambie wadau wa ngumi na wakazi wa Morogoro kuwa safari hii Twaha Kiduku atapanda ulingoni dhidi ya Iago Kiziria kutoka Georgia, tunategemea kushuhudia pambano kali na lenye ushindani mkubwa kutoka pande zote mbili," alisema na kuongeza:

"Mwaka jana wadau wa ngumi kutoka mkoani Morogoro, walitoa ushirikiano mkubwa sana kwa kuweza kuujaza Ukumbi wa Tanzanite sambamba na wakazi wa mikoa ya jirani, Dar es Salaam, Iringa, Mbeya na Dodoma, tunatarajia kushuhudia tena kuona rekodi ya mwaka jana inavunjwa kwa kuijaza Tanzanite."

Mratibu huyo alisema ukimuondoa Kiduku bado wataletea mapambano mengine makubwa na makali ya utangulizi siku hiyo ambapo Habibu Pengo atacheza na Saidi Mkola, na kwamba hiyo ni mbivu na mbichi kwa kuwa mwaka jana pambano lao lilishindika kupigwa dakika za mwisho.

"Juma Choki atacheza na Loren Japhet katika pambano ambalo tunaamini litakufa jitu, huku Ally Ngwando wa Manzese akitarajiwa kucheza na Jamal Kunoga wa Morogoro, hawa kwa sasa wapo kwenye moto katika uzito wao.

"Wengine ni Abdallah Yuba atakayepanda ulingoni dhidi Jitu Rajab, Leonard Dedan na Babu Luda, Joseph Mchapeni vs Emanuel Mbogo, James Kilian vs Waziri Magombana, Pascal Manyota vs Ahmed Pelembela, Charles Chilala vs Hamadi Furahisha na Sara Alex dhidi ya Florah Malechela, " alisema Khatibu.



Mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke (kulia), akishangilia sambamba na Pape Sakho baada ya kuifungia timu yake bao la pili kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Highland Estates, Ubaruku, Mbarali mkoani Mbeya jana na Simba kushinda mabao 2-0 yote yakifungwa na straika huyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## FA Cup 16-bora Zanzibar kupigwa Mei

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HATUA ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup, inatarajiwa kuanza kupigwa Mei 2, mwaka huu, baada ya droo ya michuano hiyo inayotoa mwakilishi wa Zanzibar kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, kufanyika jana visiwani hapa.

Katika droo hiyo iliyofanyika chini ya Kamati ya Mashindano ya ZFF na kuhudhuriwa na klabu zote 16 zilizotinga hatua hiyo, ilifanyika kwenye ukumbi wa ofisi za shirikisho hilo zilizopo Uwanja wa Amaan ambapo Mlandege imepangwa kucheza dhidi ya Muungano Rangers huku KMKM SC ikipangwa kuvaana na Villa FC.

Timu nyingine katika droo hiyo, Dulla Boys imepangwa kuvaana na New Boys huku Black Sailor ikipangwa kucheza na New City, Kundemba FC dhidi ya Mwembeladu FC, JKU dhidi ya Raskazone, Mafunzo SC dhidi ya New King na Uhamiaji dhidi ya Mwembe Makumbi City.

Kwa Upande wa pemba hatua ya robo fainali katika droo hiyo hiyo, Mkoroshoni FC itavaana na Maendeleo United, Jamhuri SC dhidi ya Chipukizi FC, Al Azar dhidi ya Tekeleza FC na Machomane itamenyana na Young Islander.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ZFF, Ali Bakar 'Cheupe', amesema ratiba ya michuano hiyo itatoka mapema leo April 11, ambapo hatua ya 16-bora kwa Unguja na hatua ya robo fainali Kwa Pemba inatarajiwa kuanza Mei 2, mwaka huu.

Alisema Kamati ya Mashindano ZFF, tayari imekamilisha matayarisho yote mama ya hatua ya 16-bora na robo fainali kwa Kanda ya Pemba.

Hata hivyo, amezitaka klabu zote zilizotinga hatua hiyo kuhakikisha zinafuata kanuni ya mashindano hayo ili kuepuka usumbufu.

**Kamati ya Mashindano ZFF, tayari imekamilisha matayarisho yote mama ya hatua ya 16-bora na robo fainali.**

# Ruvu Shooting, Polisi Tanzania zapumulia mashine

**Na Adam Fungamwango**

HALI imeendelea kuwa mbaya kwa timu za majeshi, Polisi Tanzania na Ruvu Shooting kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuendelea kufanya vibaya katika mechi zao, huku kukiwa na wasiwasi wa kushuka daraja kutokana na kuwa na pointi zisizoridhisha.

Kipigo cha mabao 3-1 ilichokipata juzi kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya dhidi ya Prisons, kimeifanya Ruvu Shooting kuendelea kupumulia mashine kwenye Ligi Kuu, ikiwa imesaliwa na mechi nne tu kumaliza msimu huu.

Ili iepuke kushuka daraja, Ruvu Shooting, yenye pointi 20 sasa italazimisha kushinda mechi zake nne zilizobaki ili kufikisha pointi 32, huku ikiombea timu zilizo juu yake zipoteze.

Imebakisha mechi nne dhidi ya Azam, Simba, Singida Big Stars na Dodoma Jiji, huku ugumu wa mechi tatu ilizonazo unazidi kuiwekwa kwenye wakati mgumu zaidi.

Mpaka sasa inakamata nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi, ikiwa kwenye hatari ya kushuka daraja moja kwa moja, huku ikihitaji kazi ya ziada ili kuweka kucheza 'play off'.

Hali ni mbaya zaidi kwa Polisi Tanzania, inayoburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 19 tu mpaka sasa ikisalia na mechi nne tu za kumalizia msimu na kujua hatma yake.

Ikishinda mechi nne zilizobaki itafikisha pointi 31, lakini ikiombea timu za juu yake zipoteze kitu ambacho ni ngumu mno timu zote kupoteza.

Bahati mbaya iliyonayo Polisi Tanzania ni kwamba, mechi nne ilizobakiza, mbili ni dhidi ya Simba na Azam FC, timu ambazo licha ya kwamba zina uwezo mkubwa na wachezaji wenye ubora, lakini zinasaka pointi tatu kwenye kila mechi kwa udi na uvumba kwa ajili ya kusaka nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao na Kombe la Shirikisho.

Mechi zingine mbili zilizobaki ni dhidi ya Ihefu na Mtibwa Sugar.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ZIYECH ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imeonesha nia ya kumsajili winga wa Morocco, Hakim Ziyech, 30, kutoka Chelsea msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### MARSCH HAITAKI LEICESTER

KOCHA wa zamani wa Leeds United, Jesse Marsch ameamua kutochukua kazi ya Leicester City licha ya kukaribia kufikia makubaliano ya mwisho ***(Telegraph)***

### BALOGUN AWINDWA MILAN

AC Milan wamemuongeza mshambuliaji wa England chini ya miaka 21, Folarin Balogun, ambaye yuko kwa mkopo Reims kutoka Arsenal kwenye orodha ya wachezaji wanaolengwa katika majira haya ya joto. ***(Calciomercato)***

### UNITED INATAKA NYOTA

KLABU ya Manchester United pia imewaweka kiungo wa kati wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo, 21, na kiungo wa kati wa Argentina, Alexis Mac Allister, 24, kwenye orodha yao fupi ya uhamisho. ***(Telegraph)***

### BENZEMA KUBAKI MADRID

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Ufaransa, Karim Benzema, 35, anataka kusalia Real Madrid kwa angalau msimu mmoja zaidi baada ya kukataa ofa kutoka Saudi Arabia. ***(Marca)***

### CHELSEA, LIVERPOOL VITANI

CHELSEA na Liverpool zinamwania Nicolo Barella, 26, wa Inter Milan huku miamba hao wa Italia wakiwa tayari kumuuza kiungo huyo wa kati wa Italia. ***(Clciomercato)***

### DISASI AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imekuwa na mazungumzo chanya na Monaco kuhusu uwezekano wa kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Axel Disasi, 25. ***(Give Me Sport)***

### PAVARD KUNG'OLEWA BAYERN

KLABU ya Manchester United inaweza kuelekeza nguvu zao katika kumsajili mlinzi wa Bayern Munich, Benjamin Pavard, 27, ikiwa miamba hao wa Ujerumani wataishinda United katika mbio za kumsajili mlinzi wa Bayer Leverkusen, Jeremie Frimpong, 22, msimu huu. ***(Football Insider)***

### RAYA HATASAINI BRENTFORD

GOLIKIPA wa Hispania, David Raya, 27, hatasaini mkataba mpya katika Klabu ya Brentford, ambao wanatazamiwa kuomba ada ya euro milioni 40 kumuuza mchezaji huyo msimu huu. (***Fabrizio Roman***o)


### RABIOT AISIKILIZIA JUVE

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot, 28, amesema bado anasubiri iwapo atasaini mkataba mpya na Juventus. Mkataba wake unaomalizika msimu huu wa majira ya joto. ***(Fabrizio Romano)***

### REUS KUJIFUNGA DORTMUND

MCHEZAJI wa Borussia Dortmund, Marco Reus, 33, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika msimu huu anatazamiwa kusaini mkataba mpya msimu ujao, ingawa atalazimika kuzungumza kukatwa mshahara. ***(Bild)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA ATAKA ARSENAL KUKOMALIA UBINGWA

**LONDON,** England

MIKEL Arteta ameitaka Arsenal kuchukua hatua yao na kusonga mbele baada ya viongozi hao wa Ligi Kuu England kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Liverpool juzi, Jumapili.

**Arsenal walionekana kuwa tayari kurejesha uongozi wao wa pointi nane dhidi ya wapinzani wao Manchester City wakati Gabriel Martinelli na Gabriel Jesus walipowapatia uongozi mzuri wa kipindi cha kwanza.**

Mohamed Salah alifunga bao na kukosa penalti, huku Roberto Firmino aliyeingia akitokea benchi akifunga bao lake la 11 la Ligi Kuu dhidi ya Arsenal - ni Harry Kane (14) na Wayne Rooney (12) pekee walio na mabao zaidi yake dhidi ya Arsenal.

Akizungumza na Sky Sports baada ya sare hiyo, Arteta alisikitika kwa kushindwa kudhibiti Arsenal kufuatia kuanza kwa kasi, lakini akakubali kuwa Liverpool walistahili kupata sare.

> ●●● Lazima tuchukue hatua, tungeweza kuchukua pointi tatu endapo tungecheza kama...

"Mchezo ulikuwa mkali sana. Mchezo ulikuwa chini ya udhibiti, lakini kabla ya muda wa mapumziko tuliruhusu bao la ovyo na mchezo ukasonga mbele," alisema Arteta.

"Ilitubidi tujipange upya baada ya muda wa mapumziko na tulianza vema katika dakika chache za kwanza, lakini tukapoteza udhibiti. Ukawa mchezo wa mpito, wenye machafuko makubwa.

"Liverpool wangeweza kufunga mabao matatu au manne. Ni kweli tungeweza kufunga mawili au matatu, hivyo labda mwisho matokeo yatakuwa ya haki.

"Tungeweza kuchukua pointi tatu. Tungecheza kama kipindi cha kwanza kwa dakika 15 nyingine na kisha mchezo ungechukua mkondo tofauti. Hatukufanya hivyo. Lazima tuchukue hatua."

Alipoulizwa kwa nini Arsenal walishindwa kudumisha ubabe wao wa mapema, Arteta alisema: "Sijaona mtu yeyote akifanya hivyo hapa. Hakuna mtu. Liverpool walishinda kila timu kubwa hapa, walicheza na Real Madrid na wangeweza kuwa nyuma kwa dakika 20.

"Watakuwa na wakati. Unahitaji kukabiliana nao na tulifanya hivyo. Kipa wetu alikuwa na sehemu kubwa katika hilo."

Matokeo hayo yanamaanisha kuwa City wako pointi sita nyuma ya Arsenal kwenye kilele wakiwa na mchezo mkononi na mechi ya nyumbani dhidi yao itapigwa Aprili 26, mwaka huu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,102,0

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 12 NA 13 APRILI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/04/23 | 22:00 | AC Milan vs Napoli | 2.64 | 3.08 | 2.59 |
| 02. 12/04/23 | 22:30 | San Lorenzo vs Boca Juniors | 2.75 | 2.65 | 2.49 |
| 03. 12/04/23 | 23:30 | Union Magdalena SM vs Deportivo Pereira | 2.23 | 2.95 | 3.21 |
| 04. 13/04/23 | 01:00 | Coritiba vs Sport Recife | 2.20 | 3.15 | 3.05 |
| 05. 13/04/23 | 01:00 | Belgrano Cordoba vs Huracan | 2.86 | 2.75 | 2.59 |
| 06. 13/04/23 | 03:30 | Rosario Central vs Independiente | 2.49 | 2.65 | 2.75 |
| 07. 13/04/23 | 03:30 | Estudiantes LP vs Atletico Tucuman | 2.20 | 2.91 | 3.32 |
| 08. 13/04/23 | 05:05 | Correcaminos Uat vs Club Celaya | 2.57 | 3.07 | 2.60 |
| 09. 13/04/23 | 19:45 | Feyenoord vs Roma | 2.24 | 3.14 | 3.19 |
| 10. 13/04/23 | 20:30 | Altay vs Altinordu | 2.18 | 3.12 | 3.02 |
| 11. 13/04/23 | 22:00 | Anderlecht vs AZ Alkmaar | 2.65 | 3.21 | 2.55 |
| 12. 13/04/23 | 22:30 | Colon Santa Fe vs Talleres | 2.65 | 2.80 | 2.44 |
| 13. 13/04/23 | 23:30 | Envigado FC vs Deportes Tolima | 2.75 | 2.70 | 2.46 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.


tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI: BUSQUETS ANAWEZA KUONDOKA BARCELONA



**BARCELONA,** Hispania

XAVI amekubali kuwa Sergio Busquets anaweza kuamua kumalizia soka lake la Barcelona kwa kiwango cha juu mwishoni mwa msimu huu, ingawa bosi huyo wa 'Blaugrana' hao ana matumaini ya kumbakisha kiungo huyo.

Busquets ameshinda mataji 31 makubwa katika kipindi cha miaka 15 akiwa na timu ya wakubwa ya Barca, lakini mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 na wababe hao wa Katalunya unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Wakati rais wa Barca, Joan Laporta, alifichua kuwa klabu hiyo ilitaka kumpa Busquets nyongeza ya mwaka mmoja mwezi uliopita, Inter Miami ya MLS imekuwa ikitajwa kwa muda mrefu kumtaka.

Barca wako pointi 12 mbele ya Real Madrid kwenye kilele cha LaLiga kabla ya kukutana na Girona jana na wakati Xavi anatumaini Busquets atasalia Camp Nou, anakubali nahodha wake anaweza kuona ushindi wa taji kama wakati muafaka wa kuondoka.

"Wacha tuone jinsi atakavyomaliza msimu," alisema Xavi kuhusu mchezaji huyo mwenzake wa zamani.

"Nimesema mara nyingi, kwangu Busquets ni muhimu sana, si tu katika mpira wa miguu, lakini pia kwenye chumba cha kubadilishia nguo.



# *Lampard ana imani na Sterling*

**LONDON,** England

FRANK Lampard amemtaka nyota wa Chelsea, Raheem Sterling, kuthibitisha kuwa bado ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani kwenye mchezo dhidi ya Real Madrid.

Fowadi huyo wa England amekuwa na wakati mgumu tangu atue hapo kwa pauni milioni 47.5 kutoka Manchester City.

Lampard alimrejesha Sterling katika mchezo wake wa kwanza akiwa kama bosi wa muda, lakini hakuweza kuwazuia 'The Blues' kuteleza kwa kuchapwa bao 1-0 na Wolves Jumamosi.

Sterling mwenye umri wa miaka 28, amefunga mabao saba pekee msimu huu, lakini akafunga bao la kwanza katika ushindi wa jumla wa 2-1 wa Chelsea dhidi ya Borussia Dortmund katika hatua ya 16-bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi uliopita.

Watakwenda Real Madrid Jumatano kwa mechi ya kwanza ya robo fainali na Lampard anatarajia mchezaji huyo wa zamani wa Liverpool kuwa bora.

Alisema: "Raheem amekuwapo na amefanya hivyo na kuna historia ya kutengeneza. Nadhani ni mchezaji mzuri.

"Amekuwa mmoja w mawinga bora zaidi d niani kwa muda mref Wakati mwingine, lab kwa maoni ya baadhi watu, bora zaidi.

"Ameinuka katika m chezo kama hiyo hap awali kwa hiyo ni jamb ambalo tutategem kwa sababu baadhi ya pengele vya kikosi lab ni vijana.

"Hakika ni mchezaji w kiwango cha juu na ana eelewa mchezo amb hautamsumbua."Yeye mchezaji wa juu. Rahee ameonyesha jinsi yeye mchezaji."

082,037/-

# SINGIDA BS YAIWEKEA YANGA KAMBI MAALUMU DODOMA

**Na Hadija Mngwai**

KUTOKANA na kuhitaji kwa udi na uvumba nafasi ya kucheza fainali ya Kombe la FA, Singida Big Stars, imesema inarudi jijini Dodoma kwa ajili ya kambi ya muda mfupi kujiandaa na mechi nusu fainali ya michuano hiyo dhidi ya Yanga.

**Singida Big Stars inatarajia kukutana na Yanga hivi karibuni katika mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA, ambapo kwa sasa wanajinadi watahakikisha wanafanikiwa kushinda mchezo huo ili watinge fainali.**

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hussein Massanza, alisema kambi yao ya Dodoma huwa inalipa kutokana na kuwasaidia kwa kiwango kikubwa hasa wanapokuwa na mechi muhimu za kuhitaji matokeo.

"Tumepokea vizuri taarifa ya kukutana na Yanga katika hatua ya nusu fainali ya Azam Sports Federation, Yanga kwa sasa wapo vizuri sana na ni bingwa mtetezi wa kombe hili, tulijipanga tangu mwanzo kukutana na timu zote kati ya Geita ama Yanga yeyote ambaye angeingia nusu fainali tunapambana naye.

"Benchi la ufundi linajipanga ili kuweza kufanya vizuri katika mchezo huu, tunajua wapinzani wetu wanafanya vizuri Ligi Kuu na kimataifa, hivyo kwa kutambua ubora wa wapinzani wetu, tumeamua kuweka kambi maalumu Dodoma.

"Tunaendelea kuweka kambi Dodoma kwa sababu ni mahali pazuri hasa tunapohitaji kuwa na umakini wa hali ya juu, hivyo tunaweka kambi hii maalumu kwa ajili ya Yanga na mechi nyingine za Ligi Kuu. Tunafurahia mchezo huu, tutauchezea nyumbani katika Uwanja wa CCM Liti, itatupa kujiamini zaidi na kupata matokeo mazuri," alisema.

Wakati Yanga itavaana na Singida Big Stars katika Uwanja wa Liti mkoani Singida, nusu fainali nyingine kati ya Simba na Azam FC, itapigwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara huku fainali ya michuano hiyo ikitarajiwa kufanyika Dimba la Mkwakwani jijini Tanga.

## Yanga yatamba

INATOKA UK. 24

sababu kuna kitu Yanga wanakihitaji na wao wamejipanga vizuri kuhakikisha wanapata matokeo chanya.

Alisema wanacheza na timu kubwa, hivyo kwa asilimia kubwa kuna faida kwao kutumia uwanja wao wa nyumbani na wako tayari kushindana kutafuta pointi muhimu dhidi ya Yanga.

"Tunawaheshimu sana Yanga, kwa sababu ya ubora wao, tutacheza kwa nidhamu ya hali ya juu, kutafuta alama muhimu lakini na kutoruhusu bao kwa wapinzani wetu," alisema Chamberi.

Kocha Msaidizi wa KMC FC, Ahmad Ally, alisema maandalizi yao ni mazuri na walijaribu kuangalia mapungufu yao na kufanyia kazi na kikosi chao kipo tayari kutafuta matokeo dhidi ya Geita.

"Tunauhitaji mkubwa wa pointi kwa sababu tunahitaji kuondoka katika nafasi ya chini kwenye msimamo, tunacheza mpira mzuri, lakini malengo makubwa ni kutafuta pointi tatu, hakuna kitu kingine zaidi katika mchezo wetu dhidi ya Geita," alisema Ahmad.

Kocha Msaidizi wa Geita Gold FC, Mathias Wandiba, alisema baada ya kupoteza dhidi ya Yanga kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la FA, wamefanyia kazi madhaifu yao na sasa wanakuja kivingine kuwakabili KMC FC.




Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van der Pluijm

## *Simba SC yanguruma*

INATOKA UKURASA 24

lake, lakini akageuka ghafla na kuachia shuti lililopanguliwa na kipa Fikirini.

Kipindi chote cha kwanza Ihefu walionekana kuwashambulia Simba, huku wageni wakijibu kwa kushtukiza.

Katika kipindi cha pili, Simba walionekana kuamka na kutulia hasa sehemu ya kati kwenye kiungo, hivyo kusukuma mashabulizi ambayo mara kwa mara yalikuwa yakizuiliwa kwa ustadi na mabeki Yahaya Mbegu, Nicolaus Wadada, na Said Nyoso.

Baadaye ilionekana ni kama mechi hiyo kuwa na uwiano sawa na mashabiki wengi kudhani ingemalizika kwa suluhu kabla mambo hayajageuka dakika za mwisho.

Kilichowaponza Ihefu baada ya kufungwa bao ni kwenda mbele kusaka la kusawazisha, ndipo waliporuhusu la pili.

Kwa matokeo hayo, Simba imefikisha pointi 60, ikiwa imecheza mechi 25, ikibakisha michezo mitano ya kumaliza msimu huku Ihefu ikibaki na pointi zake 33 kwenye nafasi ya saba.



## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/04/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Brentford FC | 2.33 | 3.10 | 2.95 |
| 02. 15/04/23 | 17:00 | Chelsea FC vs Brighton & Hove Albion | 2.41 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 15/04/23 | 17:00 | Southampton FC vs Crystal Palace | 2.60 | 3.10 | 2.60 |
| 04. 15/04/23 | 17:00 | Blackpool vs Wigan Athletic | 2.35 | 3.05 | 3.00 |
| 05. 15/04/23 | 17:00 | Queens Park Rangers vs Coventry City | 2.90 | 3.00 | 2.41 |
| 06. 15/04/23 | 17:00 | Stoke City vs West Bromwich Albion | 2.55 | 3.10 | 2.65 |
| 07. 15/04/23 | 17:00 | KAS Eupen vs SV Zulte Waregem | 2.33 | 3.40 | 2.75 |
| 08. 15/04/23 | 17:30 | Estoril Praia vs Portimonense SC | 2.38 | 3.00 | 3.00 |
| 09. 15/04/23 | 18:00 | Stade Rennes vs Stade Reims | 2.22 | 3.30 | 2.95 |
| 10. 15/04/23 | 19:15 | KV Oostende vs Oud-Heverlee Leuven | 2.48 | 3.45 | 2.50 |
| 11. 15/04/23 | 22:00 | Sparta Rotterdam vs SC Heerenveen | 2.23 | 3.30 | 2.95 |
| 12. 15/04/23 | 22:00 | America FC MG vs Fluminense FC RJ | 2.70 | 3.10 | 2.55 |
| 13. 16/04/23 | 00:30 | Botafogo FR RJ vs Sao Paulo FC SP | 2.49 | 3.05 | 2.80 |
| 14. 16/04/23 | 03:30 | Gimnasia Y Esgrima La Plata vs CA Belgrano | 2.30 | 2.75 | 2.90 |
| 15. 16/04/23 | 19:30 | Malaga CF vs FC Cartagena | 2.31 | 2.90 | 3.20 |
| 16. 16/04/23 | 20:00 | Union de Santa Fe vs CA Tigre | 2.60 | 2.85 | 2.47 |
| 17. 16/04/23 | 20:30 | VfL Wolfsburg vs Bayer Leverkusen | 2.75 | 3.35 | 2.32 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 11/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3773 | Binh Phuoc vs BA Ria Vung Tau FC | 2.87 | 2.97 | 2.35 |
| 13:00 | 5345 | Hoang Anh Gia Lai vs K. Khanh Hoa | 1.53 | 3.80 | 5.14 |
| 13:30 | 3024 | Keciorengucu vs Goeztepe | 2.18 | 3.29 | 2.88 |
| 14:00 | 2301 | Millwall U23 vs Swansea U23 | 2.20 | 4.05 | 2.51 |
| 14:00 | 4748 | M. Nam Dinh vs Song Lam Nghe AN | 2.13 | 3.12 | 3.12 |
| 14:00 | 5875 | Crewe U23 vs Charlton U23 | 2.75 | 3.99 | 2.06 |
| 15:00 | 1493 | Artsakh vs Shirak Gyumri | 2.50 | 2.99 | 2.73 |
| 15:00 | 3685 | SP. Braga U23 vs FC Famalicao U23 | 2.08 | 3.42 | 3.06 |
| 15:00 | 4975 | Gabala Fk-2 vs Moik Baku | 2.14 | 3.36 | 2.99 |
| 15:30 | 1303 | Peterborough U21 vs Barnsley U23 | 2.16 | 3.74 | 2.70 |
| 15:30 | 1370 | Geylang Int. vs Balestier Khalsa | 1.57 | 4.30 | 4.19 |
| 15:30 | 4801 | Young Lions vs Brunei Dpmm | 5.33 | 5.02 | 1.38 |
| 16:00 | 1418 | Bodrumspor vs Pendikspor | 2.37 | 3.13 | 2.72 |
| 16:00 | 3300 | KMC vs Geita Gold FC | 2.45 | 2.85 | 2.85 |
| 16:00 | 4032 | New Zealand W vs Nigeria W | 2.91 | 3.22 | 2.24 |
| 16:30 | 2222 | Persebaya Surabaya vs Arema | 2.04 | 3.33 | 3.13 |
| 17:00 | 1039 | FC Vizela U23 vs Estoril Praia U23 | 2.34 | 3.47 | 2.59 |
| 17:00 | 1983 | Vojvodina vs Novi Pazar | 1.67 | 3.49 | 4.42 |
| 17:00 | 2828 | SK Super Nova vs FS Metta/Lu | 2.75 | 3.32 | 2.29 |
| 17:00 | 4220 | Portimonense U23 vs CD Mafra U23 | 1.46 | 4.35 | 5.39 |
| 17:00 | 5114 | BFC Daugavpils vs Valmiera Fk/Bjss | 6.85 | 4.57 | 1.36 |
| 17:30 | 4505 | Italy W vs Colombia W | 1.36 | 4.26 | 7.69 |
| 17:45 | 1415 | MC Magra vs MC Alger | 2.61 | 2.71 | 2.87 |
| 18:00 | 1069 | Urartu vs Pyunik Yerevan | 2.43 | 2.96 | 2.85 |
| 19:00 | 2064 | CSA Steaua Bucuresti vs FC Politehnica Iasi | 2.17 | 3.13 | 3.03 |
| 19:00 | 4230 | Germany W vs Brazil W | 1.37 | 4.34 | 7.03 |
| 19:00 | 4299 | Omonia Nicosia vs Aris Limassol | 3.16 | 3.31 | 2.17 |
| 19:00 | 4305 | Young Africans vs Kagera Sugar | 1.20 | 5.29 | 11.76 |
| 19:00 | 4751 | Pafos FC vs AEK Larnaca | 2.37 | 3.23 | 2.86 |
| 19:00 | 5246 | GKS Katowice vs OKS Odra Opole | 1.92 | 3.34 | 3.44 |
| 19:30 | 1629 | Silkeborg vs Horsens | 1.63 | 3.85 | 4.96 |
| 20:00 | 4248 | Tennis Borussia Berlin vs Lokomotive Leipzig | 5.80 | 3.75 | 1.43 |
| 20:30 | 4279 | Samsunspor vs Tuzlaspor | 1.35 | 4.50 | 6.76 |
| 21:30 | 5766 | Gornik Leczna vs LKS Lodz Pss | 3.03 | 3.13 | 2.17 |
| 21:45 | 1008 | Peterhead vs Dunfermline | 8.13 | 4.90 | 1.30 |
| 21:45 | 1060 | Dundee FC vs Raith Rovers | 1.51 | 4.01 | 5.42 |
| 21:45 | 1382 | Dumbarton vs Stirling | 2.72 | 3.23 | 2.31 |
| 21:45 | 2070 | Portadown FC vs Newry City AFC | 1.86 | 3.39 | 3.60 |
| 21:45 | 3208 | Glenavon vs Ballymena Utd | 1.78 | 3.55 | 3.75 |
| 21:45 | 3441 | Cliftonville Belfast vs Larne | 3.28 | 3.08 | 2.08 |
| 21:45 | 3734 | Montrose vs Falkirk FC | 3.02 | 3.49 | 2.09 |
| 21:45 | 4044 | Elgin City vs Stenhousemuir | 2.67 | 3.19 | 2.37 |
| 21:45 | 4669 | Morton vs Hamilton | 1.69 | 3.64 | 4.36 |
| 21:45 | 4906 | Crusaders Belfast vs Coleraine FC | 1.87 | 3.33 | 3.64 |
| 21:45 | 4981 | England W vs Australia W | 1.41 | 4.25 | 6.43 |
| 21:45 | 5263 | Inverness vs Arbroath | 2.15 | 3.13 | 3.23 |
| 22:00 | 1502 | Al Khaleej Club vs Al Shabab Riyadh | 5.95 | 4.36 | 1.49 |
| 22:00 | 3383 | Manchester City vs Bayern Munchen | 1.77 | 3.69 | 3.93 |
| 22:00 | 5996 | Benfica vs Inter | 2.10 | 3.20 | 3.31 |
| 22:10 | 2291 | France W vs Canada W | 1.36 | 4.45 | 7.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Aprili 11, 2023

Nipashe




Lampard ana imani na Sterling UKURASA 22

SHUTI...



Mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke, akiachia shuti katikati ya mabeki wa Ihefu FC, Nicholas Wadada (chini) na Samwel Onditi, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa katika Uwanja wa Highland Estates, Ubaruku, Mbarali mkoani Mbeya jana na Simba kushinda mabao 2-0 yote yakifungwa na straika huyo. **MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA SC YANGURUMA ALIPOFIA MWANANCHI

## ●●● Ni yule yule Baleke, aiongoza kuitafuna tena Ihefu akiweka rekodi mpya ya...

**Na Adam Fungamwango**

JEAN Beleke, straika kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, ameiongoza tena Simba kuitafuna Ihefu FC, safari hii akiiwezesha kunguruma katika Uwanja wa Highland Estates, Ubaruku, Mbarali mkoani Mbeya, alipofia 'Mwananchi' (Yanga).

**Baleke ameweka rekodi ya kipekee kwa kuifunga timu moja mabao matano katika mechi mbili mfululizo, hiyo ikiwa ni baada ya kutupia matatu 'hat-trick' kwenye ushindi wa 5-1 mchezo wa robo fainali wa] Kombe la FA, Jumamosi iliyopita na jana kucheka tena na nyavu mara mbili wakati Simba ikishinda 2-0 nyumbani kwa Ihefu mechi ya Ligi Kuu Bara.**

Straika huyo aliyesajiliwa na Simba kipindi cha dirisha dogo la usajili anatimiza mabao 14 tangu ajiunge na timu hiyo, huku akiwa amefikisha mabao saba kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, matano kwenye Kombe la FA na matatu Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba pia imevunja rekodi ya Ihefu kuzifunga timu zote za Dar es Salaam ambazo zimekanyagaga kwenye uwanja wa huo kwani Novemba 29, mwaka jana iliibamiza Yanga mabao 2-1, ikaichapa KMC 1-0 Januari 3, mwaka huu, kabla ya kuidungua Azam FC bao 1-0 Machi 13, mwaka huu.

Mchezo wa jana ilionekana ni kama Ihefu wameshaikamata Simba, lakini dakika saba kabla ya mechi kumalizika hali kwenye uwanja huo ikabadilika.

Krosi ya Israel Mwenda ilileta kizaazaa kwenye lango la Ihefu, na mpira uliokuwa ukizagaa langoni ulimkuta Baleke ambaye alipiga shuti hafifu la mguu wa kushoto, pembeni mwa kipa Bakari Fikirini aliyekuwa akikingwa na mabeki wake, mpira ukajaa wavuni kulia kwake.

Wakati mashabiki wa Simba waliojazana kwenye uwanja huo wakiendelea kushangilia bao hilo, dakika ya 86, ikiwa ni dakika tatu baada ya bao la kwanza, walilazimika kusimama tena kushangilia bao maridadi la Beleke alilolifunga kwa staili ya kubinjuka 'acrobatic'.

Alikuwa ni Kibu Denis aliyeukimbilia mpira mrefu wingi ya kulia, akapiga krosi ambayo ilitua kwenye kichwa cha straika huyo akapiga kichwa, mpira ukagonga nguzo ya juu na kurejea uwanjani, akaruka juu na kubinuka sarakasi akaupiga tena kwa mguu huku akijipindua, akiandika bao la pili lililoendelea kuzua shangwe kwa mashabiki dimbani hapo.

Katika mchezo huo, ulianza kwa Ihefu kulishambulia lango la Simba kama nyuki na kuwafanya mabeki wa timu hiyo na kipa wao Ally Salum kuwa 'bize' muda mwingi wa mchezo.

Ismael Sawadogo, dakika ya 16 alianguka mwenyewe katika juhudi za kutaka kuumiliki mpira, ukapitiwa na Yacouba Songne ambaye alivuta hatua mbili tu kabla ya kuachia kombora la chini lililookolewa kwa kupanguliwa kwa ustadi na Salim, ikawa kona.

Simba ilijibu shambulizi hilo dakika moja baadaye likiwa ni la kwanza tangu kuanza kwa mechi hiyo, pale Jean Baleke alipoupata mpira akiwa anaangalia kwenye lango

INAENDELEA UKURASA 23

## Yanga yatamba kikosi kipana kwa Kagera Sugar leo

**Na Saada Akida**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikitarajiwa kuendelea leo katika viwanja viwili Dar es Salaam, mabingwa watetezi, Yanga wamesema wanajivunia kikosi kipana wakiikaribisha Kagera Sugar katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam mechi itakayochezwa saa 1:00 usiku.

Mchezo mwingine leo utakuwa kati ya KMC FC watakaoikaribisha Geita Gold FC katika Uwanja wa Uhuru saa 10:00 alasiri.

Kuelekea michezo hiyo makocha wa timu hizo wamezungumza na Nipashe na kutoa tathimini zao, ambapo Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema muda wa maandalizi ni tatizo kutokana na mazingira kuwalazimu kucheza kila baada ya siku tatu, lakini wataitumia mechi ya leo kutengeneza wachezaji wao kiakili.

Alisema mechi haitakuwa rahisi kwa sababu awali walicheza Mwanza na kushinda kwa tabu bao 1-0 na kwamba Kagera Sugar walipata penalti, lakini kipa wao alikuwa makini na kuidaka.

"Mechi haitakuwa rahisi, kwa hali hiyo kutakuwa na mabadiliko katika kikosi kwa sababu ya kuwapumzisha waliocheza juzi na mabadiliko hayo hayataathiri kikosi ambacho tutakishusha kutafuta matokeo mazuri.

"Kwa sasa kikosi kimekuwa kipana kwa sababu baadhi ya majeruhi wamerejea na tutawapa nafasi taratibu akiwamo Bernard Morrison ambaye anatakiwa kupewa dakika chache za kucheza ili kumrejesha kwenye ubora wake," alisema Kaze.

"Mwakilishi wa wachezaji wa Yanga, Denis Nkane, alisema wako tayari kwa mchezo wa leo na wanatambua haitakuwa mechi rahisi kwa sababu ya ubora wa Kagera Sugar ambao nao wanakuja kwa malengo yao.

Kocha Msaidizi wa Kagera Sugar, Marwa Chamberi, alisema mchezo utakuwa mgumu kwa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >